


*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima, wakati wa uzinduzi wa Mkakati wa Jubilei wa World Vision Tanzania wa miaka mitano (2026–2030) unaolenga kuboresha ustawi na maendeleo endelevu ya watoto, familia na jamii nchini jijini Dar es Salaam tarehe 25 Februari 2026.*

KIMEPIGWACHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI, DODOMA-TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# HOTUBA YA MHE. DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB), WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27






*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima, akionesha Kitabu cha Mkakati wa Kitaifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji nchini (2025/2026–2029/2030) aliouzindua katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji yaliyofanyika Februari 12, 2026, Wilaya ya Monduli Mkoani Arusha.*



*Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi akijenga kuashiria kuanza kwa ujenzi wa Makazi Bora katika Wilaya ya Misungwi Mkoani Mwanza tarehe 23 Desemba, 2025.*

# VIONGOZI WAKUU WA WIZARA



Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)
**WAZIRI**



Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb)
**NAIBU WAZIRI**



Eliakim Chacha Maswi
**KATIBU MKUU**



Wakili Amon Mpanju
**NAIBU KATIBU MKUU**



Felista Mdemu
**NAIBU KATIBU MKUU**

# HOTUBA YA MHE. DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB), WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka 2025/26 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2026/27. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ili kuwasilisha hotuba yangu. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua tena kuiongoza Wizara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa Nchi yetu. Natambua kuwa, Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona utoaji wa huduma za

ustawi na maendeleo ya jamii; malezi na makuzi ya watoto; na uwezeshwaji kiuchumi kwa makundi maalum unafanyika kwa kasi na ufanisi mkubwa. Ninaahidi kwamba Wizara itaendelea kutimiza majukumu yake kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

***SALAMU ZA PONGEZI***

3. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa tena na Watanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuendelea kuongoza nchi yetu kwa kipindi kingine. Aidha, ninapenda kumpongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawaombea viongozi wetu afya njema, hekima na mafanikio katika kuwatumikia watanzania.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Ninampongeza kwa uongozi wake madhubuti na juhudi zake za kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii. Tunatambua na kuthamini mchango wake

mkubwa katika kuimarisha ushiriki wa wanaume katika kukuza usawa wa kijinsia kupitia kampeni ya "***He for She***".

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb),** kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa 12 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe **1 Aprili, 2026** ambayo imeainisha vipaumbele na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2026/27.

6. ***Mheshimiwa Spika***, ninakupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilala na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb),** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge, **Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb**), **Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb)** na **Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso (Mb)** kwa umakini wao katika kusaidia kuongoza vikao vya Bunge. Ninawaombea na kuwatakia kazi njema katika majukumu yenu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, pia ninapenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya **Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma (Mb)** na **Makamu wake, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima (Mb)** kwa ushauri na maelekezo yao wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Hakika, ushauri na maelekezo ya Kamati yamekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha utendaji wa Wizara. Aidha, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara yangu kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa afua za maendeleo na ustawi wa jamii nchini.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Ni ahadi yangu kwamba, Wizara itaendelea kushirikiana nao kwa karibu ili kuhakikisha tunatekeleza kwa vitendo maono na dhamira ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa na jamii yenye ustawi na maendeleo jumuishi na endelevu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninamshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi (Mb),** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa

anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Amekuwa msaada mkubwa katika kusimamia shughuli za Wizara, kutoa ushauri na kuhakikisha utekelezaji wa majukumu unafanyika kwa ufanisi. Hakika, wanawake wa Mkoa wa Mbeya hawakukosea kumchagua kuwa mwakilishi wao.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninaishukuru Menejimenti na Wataalam wote wa Wizara wakiongozwa na **Bw. Eliakim Chacha Maswi,** Katibu Mkuu na wasaidizi wake **Wakili Amon Anastaz Mpanju,** Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum na **Bi. Felista Peter Mdemu**, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Jinsia na Wanawake kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mkubwa unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu.

***SALAMU ZA POLE***

12. ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa pole kwa kuondokewa na wabunge wenzetu, **Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb)** na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); **Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa **Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi)**, waliotoa mchango mkubwa katika Taifa kupitia Bunge na Serikali. Tunawaombea pumziko la amani na tunawakumbuka kwa utumishi uliotukuka.

13. ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa pole kwa kifo cha **Mheshimiwa Julie Catherine Manning**, mwanamke wa kwanza Tanzania kusoma Shahada ya Sheria na kuhudumu kama Jaji wa Mahakama Kuu katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, pamoja na kuwa Waziri wa kwanza wa Sheria mwanamke.

Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, wadau na Watanzania wote walioguswa na vifo hivyo kwa namna moja au nyingine. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa marehemu pumziko la amani. Amina!

14. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa utangulizi huu, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu Maono ya Kimageuzi katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/26, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya kimkakati vya Wizara kwa mwaka 2026/27.

**MAONO YA KIMAGEUZI KATIKA SEKTA YA MAENDELEO NA USTAWI WA JAMII**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu imebeba ujumbe mkuu kwamba, Maendeleo ya Taifa hayawezi kupimwa kwa miundombinu pekee, bali kwa **ubora wa maisha ya watu**; **uimara wa jamii**; **usalama wa kijamii**; **ushiriki wa wanawake katika maendeleo**; **ustawi wa watoto na wazee pamoja na uwezo wa wananchi kushiriki kikamilifu katika kujiletea Maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.** Hapa pia napenda kunukuu maneno ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** alipotoa Hotuba yake ya kufungua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba 2025, Dodoma alisema nanukuu "**Namuomba Mungu kuwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe tu kwa vitu bali pia, kwa**

**Tabasamu la Utu litakaloachwa kwenye nyuso za Watanzania”**. Mwisho wa kunukuu.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa msingi huo, Wizara hii ni mhimili mahsusi wa maendeleo ya watu na injini ya uchumi jumuishi nchini. Aidha, ni nyenzo ya kuleta mageuzi ya fikra katika jamii ambayo ni msingi muhimu katika kufanikisha DIRA 2050 yenye lengo la kujenga Taifa lenye Demokrasia, Haki na Uhuru; Taifa linalozingatia Utu; Amani na Umoja. Taifa lenye uwezo wa kumiliki na kutumia kikamilifu rasilimali zake kwa manufaa ya wananchi pamoja na kuhifadhi, kukuza na kulinda maadili na tamaduni chanya za kitanzania.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii ninayoiwasilisha haiainishi tu takwimu za kibajeti, bali inaeleza maono na mwelekeo wa Taifa katika kujenga Taifa lenye ustawi, Mshikamano, maadili na ushiriki mpana wa wananchi katika maendeleo. Tunaamini kwamba, maendeleo ya kweli na endelevu hayawezi kupatikana kwa ukuaji wa uchumi pekee bila kuwa jamii imara inayojali makundi yote ya wananchi na inayowezesha kila mmoja kushiriki katika kujiletea maendeleo. Kwa mantiki hiyo, Sekta hii ni ya kimkakati na kimageuzi inayojenga msingi wa Taifa lenye watu wenye utu, uwajibikaji, uzalendo na

uwezo wa kuchangia kikamilifu katika kufikia malengo ya DIRA 2050.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** mwelekeo wa Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa jamii unajengwa katika misingi ya kutambua kuwa watu ndiyo rasilimali kuu ya Taifa. Kwa msingi huo, wanawake ni nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, watoto ni msingi wa Taifa la kesho, wazee ni hazina ya Taifa na jamii imara ndiyo nguzo ya amani, mshikamano na maendeleo endelevu. Aidha, Wizara inaendelea kutambua na kuthamini mchango wa makundi mbalimbali ya wananchi wakiwemo machinga, bodaboda, mama/baba lishe pamoja na wafanyabiashara ndogondogo wengine ambayo ni sehemu muhimu ya uchumi rasmi wa Taifa.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kusisitiza kwamba, msingi mkuu wa DIRA 2050 unaojengwa juu ya Utawala bora, Amani, Usalama na Utulivu si kauli ya kawaida ya sera, bali ni uamuzi wa kimkakati wa Taifa letu unaoendelea kuimarishwa na uongozi madhubuti wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kuonesha kwa vitendo nafasi muhimu ya mwanamke kwa maendeleo ya Taifa. Hali hiyo imejidhihirisha katika DIRA 2050 inayolenga kupunguza pengo la kijinsia

kwa angalau asilimia 85 na kuiwezesha Tanzania kuwa kinara Barani Afrika na kuwa miongoni mwa nchi 10 bora Duniani.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** kuelekea DIRA 2050 tunategemea kujenga Tanzania ya wanawake na wanaume wenye uwezo sawa wa kushiriki, kuamua, kumiliki, kuzalisha, kuongoza na kunufaika na maendeleo ya Taifa. Kwa mtazamo wa kimkakati, DIRA 2050 inabainisha kuwa usawa wa kijinsia si ajenda ya kijamii tu, bali ni ajenda ya kimageuzi ya kiuchumi (Economic Transformation Agenda) na ajenda ya kitaifa ya ushindani (National Competitiveness Agenda).

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Sheria, Mipango, Mikataba na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 (Toleo la Mwaka 2024); Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); na Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Aidha, Wizara inazo sheria tatu (3) inazozitekeleza

ambazo ni Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56; na Sheria ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Sura ya 110.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2025/26, umezingatia miongozo mbalimbali ya Taifa na Kimataifa. Baadhi ya miongozo hiyo ni pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 – 2025/26); Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya II (MTAKUWWA II, 2024/25 – 2028/29); Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi (Bottom Up 2022/23 - 2025/26); Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM 2021/22 – 2025/26); Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (2021/22 - 2024/25); Mkakati wa Taifa wa kutokomeza Ukeketaji (2021/22 – 2024/25); Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 – 2026/27); Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals, 2030*); na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza

majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum – GEF, 2021 – 2026).

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii kwa mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa katika ngazi ya msingi;

ii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii ikiwa pamoja na kukuza usawa wa kijinsia, kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi na upatikanaji wa malezi bora katika familia;

iii) Kutambua, kuratibu na kuimarisha maendeleo na ustawi wa makundi maalum wakiwemo watoto, wazee na wafanyabiashara ndogondogo;

iv) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na

v) Kuimarisha mazingira ya ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

**Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara (Fungu 53)**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni tisa, milioni arobaini, mia moja ishirini na tisa elfu** (shilingi 9,040,129,000) kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Vyanzo hivyo ni pamoja na Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Ada za Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo hivyo; Ada za Mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Ada za usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,570,588,691.45** sawa na **asilimia 39.50** ya lengo la makusanyo ya mapato. Hata hivyo, miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikiwa kwa lengo hilo ni pamoja na uhaba na uchakavu wa miundombinu katika Vyuo; kuongezeka kwa fursa mbalimbali za mikopo zenye masharti nafuu kutoka sekta binafsi na sekta ya umma; na kupungua kwa ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutokana na

mabadiliko ya sera za nchi wafadhili. Aidha, Wizara inaendelea na jitihada za kukusanya mapato katika kipindi kilichobaki ili kufikia lengo la makusanyo yaliyokadiriwa kwa mwaka 2025/2026.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu **Shilingi 76,057,153,000** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 49,115,697,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 26,941,456,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 22,646,148,000** ni Mishahara na **Shilingi 26,469,549,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo, kiasi cha **Shilingi 15,415,404,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 11,526,052,000** ni fedha za nje.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2026, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 60,459,559,340.07**, sawa na **asilimia 79.49** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 40,740,367,581.40** sawa na **asilimia 82.95** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 19,719,191,758.67** sawa na **asilimia 73.19** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika ***Jedwali Na. 1.***

***Jedwali 1***: Fedha zilizopokelewa katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026.

| **Eneo** | **Fedha zilizoidhinishwa** | **Fedha zilizotolewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida** | | | |
| Mishahara | 22,646,000,000.00 | 18,548,952,761.00 | 81.91 |
| Matumizi mengineyo | 26,469,549,000.00 | 22,191,414,820.40 | 83.84 |
| **Jumla Ndogo (a)** | **49,115,549,000.00** | **40,740,367,581.40** | **82.95** |
| **Fedha za Miradi ya Maendeleo** | | | |
| Fedha za Ndani | 15,415,404,000.00 | 13,400,000,000.00 | 86.93 |
| Fedha za Nje | 11,526,052,000.00 | 6,319,191,758.67 | 54.83 |
| **Jumla Ndogo (b)** | **26,941,456,000.00** | **19,719,191,758.67** | **73.19** |
| **JUMLA KUU** | **76,057,005,000.00** | **60,459,559,340.07** | **79.49** |

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)

28. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo imetekeleza vipaumbele vilivyoanishwa katika bajeti ya mwaka 2025/26. Utekelezaji huo umewezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali katika maeneo ya maendeleo na ustawi wa jamii kama ifuatavyo: -

## ENEO LA 1: KUENDELEZA RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA MAENDELEO NA USTAWI WA JAMII

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa rasilimali watu ni msingi muhimu katika kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma bora za maendeleo na ustawi wa jamii. Ili kufanikisha lengo la kuwa na sekta yenye ufanisi, uwajibikaji inayozingatia mahitaji ya wananchi, Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kuimarisha uwezo wa watumishi kupitia ajira mpya, mafunzo ya kitaaluma ya muda mfupi na mrefu yanayotolewa ndani na nje ya nchi. Aidha, kuimarisha programu za kuendeleza ujuzi na weledi na kuhimiza maadili ya utumishi wa umma.

## WIZARA

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imeendelea kuimarisha rasilimali watu kwa kuajiri watumishi 17 na hivyo kuwa na jumla ya **watumishi 685**. Aidha, Wizara imewathibitisha kazini watumishi 108, imewapandisha vyeo watumishi 76. Vilevile, imepokea Watumishi 25 waliohamia kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na kuhamisha watumishi 13 kwenda taasisi nyingine.

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho, Wizara imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa **watumishi 25** na mafunzo ya muda mfupi kwa **watumishi 31** katika fani mbalimbali ndani ya nchi. Aidha, kwa mwaka 2025/26 jumla ya **watumishi 17** wamestaafu kwa mujibu wa Sheria na taratibu za utumishi wa umma.

## TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ina jumla ya **watumishi 241**. Katika mwaka 2025/26 Taasisi hiyo imeajiri **watumishi 23**, watumishi nane (8) wamehamia kutoka taasisi mbalimbali na watumishi saba (7) wamehama kwenda taasisi nyingine. Aidha, Taasisi imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa **watumishi 45** ikiwemo mafunzo ya ngazi ya Shahada ya Uzamivu (PhD).

## TAASISI YA USTAWI WA JAMII

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii ina jumla ya **watumishi 192**. Katika mwaka 2025/26, Taasisi ya hiyo imeajiri **watumishi wawili (2)** na kuwathibitisha kazini **watumishi wawili (2)**. Aidha, imewapandisha vyeo **watumishi saba (7)**, imemteua mtumishi mmoja katika nafasi ya uongozi, imepokea watumishi saba (7) waliohamia kutoka taasisi mbalimbali na kuwahamisha watumishi watano (5)

kwenda taasisi nyingine. Hata hivyo, watumishi wanne (4) wamestaafu kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi wa umma.

**ENEO LA 2: MAENDELEO YA JAMII**

34. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI inatekeleza Kampeni ya Mageuzi ya Kifikra na Mitazamo ya Jamii kwa kujenga fikra na mitazamo chanya inayowezesha wananchi kufanya kazi kwa bidii, kuongeza uwajibikaji, kuwa wazalendo, waadilifu, wabunifu na wenye moyo wa kujitolea. Lengo likiwa ni kuondoa mitazamo hasi kama utegemezi, kutotumia fursa, kukosa maadili, uzalendo na kutowajibika inayosababisha kutopata maendeleo yanayotarajiwa. Kampeni hiyo inakuza ari ya wananchi kushiriki katika kuibua, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia shughuli za maendeleo na kuwafanya kuwa kitovu cha maendeleo yao na kuhakikisha miradi ya maendeleo wanayoitekeleza ni endelevu na jumuishi.

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI ilitekeleza Kampeni ya Amsha Ari katika mikoa minne (4) na kufanya jumla ya Mikoa 21 iliyofikiwa na kampeni hii. Kampeni hiyo ilifanyika kwa kushirikisha viongozi mbalimbali kuanzia ngazi

ya kata hadi Taifa ili kuonesha kwa vitendo umuhimu wa jamii kushiriki na kuchangia kwa hiari katika miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao. Kampeni hiyo ilifanyika katika Mikoa ya Mbeya - Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Mara - Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Morogoro - Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Mwanza - Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na Manispaa ya Ilemela.

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika kampeni hiyo, jumla ya wananchi **7,184** (Wanaume 3,190 na Wanawake 3,994) walishiriki wakiwemo Viongozi wa Dini, Wazee wa Mila, Watu Maarufu, Vijana, Wajumbe wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, Wafanyabiashara Ndogondogo, wajumbe wa kikundi cha Baponyamaswa na Wanafunzi wa Vyuo vya Buhare na Misungwi. Kampeni hiyo imeimarisha mshikamano wa jamii katika kufanya kazi kwa pamoja, kuongeza uelewa na uwajibikaji wa wananchi katika kusimamia na kuendeleza miradi yao, kupunguza utegemezi kwa kuimarisha ari ya wananchi kujitegemea.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI imeendelea kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kutambua umuhimu wao mkubwa katika kuamsha ari ya jamii kushiriki katika masuala ya Maendeleo yao na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Katika

mwaka wa fedha 2025/26 Maafisa Maendeleo ya Jamii **830** wameajiriwa na kufanya jumla yao kuwa **4,806** sawa na **asilimia 89.8** kati ya mahitaji ya watumishi **5,352** wanaohitajika nchi nzima.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii hao ambao wengi wao wapo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wameendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika mikoa 26 ya Tanzania Bara. Hadi kufikia Aprili, 2026 miradi ya maendeleo imeongezeka kutoka **31,802** hadi kufikia **38,443**, ikiwemo miradi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya **1,632**, ujenzi wa madarasa ya shule za awali na msingi **26,467** na madarasa ya shule za sekondari **10,344**.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI inaendelea kuratibu Kampeni ya Ujenzi wa Nyumba Bora kupitia Kaulimbiu isemayo "**Piga Kazi, Boresha Makazi".** Kupitia Kampeni hiyo, Maafisa Maendeleo ya Jamii wamehamasisha ujenzi wa nyumba bora **944** zenye gharama nafuu na hivyo kufanya jumla ya nyumba bora zilizojengwa katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kufikia **15,296** tangu kuanza kwa kampeni hiyo mwaka 2022.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kuhuisha Mwongozo wa Majukumu ya Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Mwaka 2018 na kuandaa Toleo la Mwaka 2026. Mwongozo huo umeboreshwa ili kuwawezesha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao ikiwemo uratibu na utekelezaji wa Sera mbalimbali za Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwongozo huo umejumuisha majukumu na muundo mpya wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Kitengo cha Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Mkoa kimeanzishwa na hivyo kuwezasha utekelezaji wa majukumu ya Maafisa Maendeleo ya Jamii kufanyika kwa ufanisi zaidi.

***Mheshimiwa Spika, ninatoa Shukrani za kipekee kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia uundwaji wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa ambacho kimeongeza ufanisi katika utendaji kazi na baadaye kinatarajiwa kuwa sehemu inayojitegemea.***

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na zoezi la kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996, ili iendane na hali halisi ya sasa kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Tathmini ya utekelezaji wa Sera hiyo imeonesha kuwa kuna umuhimu wa kuihuisha Sera hiyo. Wizara imekamilisha Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996, Toleo la mwaka 2026 ambayo imewasilishwa kwa wadau ili kupata maoni na inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/27.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa Sera hiyo, kutajenga msingi wa kutungwa kwa Sheria mahsusi ya wataalam wa maendeleo ya jamii. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine itaimarisha usimamizi na udhibiti wa maadili, weledi na uwajibikaji wa wataalam hao ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi.

44. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia Vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Jamii ambavyo ni Ruaha (Iringa), Rungemba (Iringa), Uyole (Mbeya), Mlale (Ruvuma), Buhare (Mara) na Monduli (Arusha); pamoja na Vyuo viwili (2) vya Maendeleo ya Jamii Ufundi ambavyo ni Misungwi (Mwanza) na Mabughai (Tanga). Katika mwaka wa masomo 2025/26 Vyuo

hivyo vimedahili jumla ya wanafunzi **5,152 (Wanaume 1,683** na **Wanawake 3,469)**

45. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza thamani na ubora wa wahitimu wa Taasisi na Vyuo, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa dhana ya uanagenzi ambayo inawaunganisha wanafunzi na taasisi, Mashirika au Kampuni kwa ajili ya kuongeza ujuzi wanaohitaji. Aidha, iliratibu utekelezaji wa dhana ya ushirikishwaji jamii, ambapo wanafunzi kwa kushirikiana na wakufunzi na jamii inayozunguka Vyuo wanaibua changamoto zilizopo katika jamii husika na kuainisha mbinu za kuzitatua. Vilevile, iliwezesha utekelezaji wa dhana ya ubunifu ambayo inawawezesha wanafunzi kutoa mawazo yao ya kibunifu ambayo yanasaidia kutatua changamoto za jamii.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya wanafunzi 180 wameunganishwa na Taasisi mbalimbali kama vile Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kwa ajili ya mafunzo ya uanagenzi. Kupitia dhana hiyo wanafunzi wameweza kupata ujuzi katika maeneo ya uandishi na usimamizi wa miradi, uanzishaji wa biashara na matumizi ya teknolojia mbalimbali.

47. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Vyuo inatekeleza programu ya ushirikishwaji jamii inayolenga kuiwezesha jamii kutatua changamoto zinazoikabili kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao. Katika mwaka 2025/26, jumla ya wananchi 1,499 walinufaika na programu hiyo kupitia mafunzo mbalimbali kama vile ushonaji, kilimo cha parachichi, lishe bora na elimu dhidi ya ukatili. Aidha, kupitia programu hii Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale kiliwakatia Bima za Afya watoto 65 wa kituo cha watoto yatima cha Chipole pamoja na kuwapatia chakula na vifaa vya shule.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya mawazo 9 ya kibunifu yameibuliwa kwenye Taasisi na vyuo hivyo, hivyo kufanya mawazo yaliyoibuliwa tangu kuanzishwa kwa vituo vya ubunifu mwaka 2019 kufikia mawazo 53; kati ya hayo, mawazo 21 yako hatua ya dhana (*Ideation)*, mawazo 13 yako katika hatua ya uatamiaji, mawazo 9 yako hatua ya sampuli kifani, na mawazo 10 yamekamilika na kuwa bidhaa na huduma kama vile:- niuzie *point of sale* – POS (Tengeru) ambao ni mfumo wa kijasiriamali unaowezesha wajasiriamali kutunza kumbukumbu za mauzo, matumizi na manunuzi; na mfumo wa kielekroniki wa *connect* (Tengeru) ambao

umesaidia kusajili wajasiriamali wanawake Mkoani Arusha.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** pia mawazo mengine ambayo tayari ni bidha ni mitungi inayotengenezwa kwa saruji (Misungwi) ambayo inatumika kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi pamoja na kifaa cha kugundua madini ardhini (Misungwi) ambacho kitawawezesha wachimbaji wadogo kutambua maeneo yenye madini. Vilevile, kuna wazo la karata lishe na draft lishe (Rungemba) ambalo linatumika kuelimisha na kuhamasisha jamii kutumia vyakula bora.

50. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ruaha, Rungemba, Mlale na Monduli imeendelea kutoa mafunzo ya ushonaji kwa wanafunzi na wananchi ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya wanafunzi na wananchi 399 wamenufaika. Mafunzo haya yameendelea kuwavutia wadau mbalimbali wakiwemo Shirika la *SOS Children's Villages Tanzania* ambalo limewezesha wasichana 26 waliopata watoto katika umri mdogo kupata mafunzo hayo katika Chuo cha Rungemba. Wasichana hao wanapatiwa ujuzi wa ushonaji ili waweze kujikwamua kimaisha, kuwalea watoto wao vema pamoja na kuepukana na vitendo vya ukatili. Mafunzo haya yanafanyika kwa kutumia vyerehani 258 vilivyopatikana kwa ushirikiano na Ubalozi wa China.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi na Mabughai imeendelea kuwajengea ujuzi na uzoefu wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo hivyo kwa kutekeleza mafunzo kwa vitendo. Aidha, vyuo hivyo vimekuwa vikitoa huduma ya usimamizi elekezi (consultancy) kwa miradi ya ujenzi na ukarabati wa taasisi za Wizara kama vile mahabusu ya watoto Bukumbi na hosteli za wasichana katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Monduli na Uyole. Usimamizi huo umesaidia kuipunguzia gharama Wizara na kuongeza uzoefu kwa wanafunzi na wakufunzi wa vyuo hivyo.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na mchakato wa kuviunganisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ili viweze kujiendesha kiutendaji (autonomous). Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara ilishirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kufanya upembuzi yakinifu wa rasilimali watu, miundombinu na taaluma katika Vyuo hivyo. Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha kuwa kuna manufaa kupitia muunganiko huo ikiwemo kupunguza utegemezi wa rasilimali fedha kutoka Serikali Kuu pamoja na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Aidha, Wizara imepokea maoni ya wadau muhimu wakiwemo Wizara ya

Fedha, OR - UTUMISHI na Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao kwa pamoja wameunga mkono azma hiyo. Hivyo, muunganiko huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/27.

## ENEO LA 3: UTAMBUZI, URATIBU NA UENDELEZAJI WA WAFANYABIASHARA NDOGONDOGO

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na shughuli za utambuzi, uratibu na usimamizi wa programu za kuwezesha Makundi Maalum kiuchumi. Makundi hayo yanajumuisha wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo machinga; mama na baba lishe; waendesha bodaboda na bajaji; wasusi; washonaji wa nguo na wafanyabiashara ndogondogo wengine wenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne (4) kwa mwaka. Makundi hayo yanalengwa kwa kuwa yanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kutofikiwa na fursa za kiuchumi kama elimu ya ujasiriamali, mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha na maeneo wezeshi ya kufanyia biashara zao.

54. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha juhudi za Serikali za kuwatambua na kuwarasimisha wafanyabiashara ndogondogo nchini, Wizara imeendelea na utekelezaji wa zoezi la utambuzi na usajili wao kupitia Mfumo wa Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo (WBN-

MIS). Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 56,039 (Wanaume 25,589 na Wanawake 30,450) wamesajiliwa na kufanya jumla ya Wafanyabiashara ndogondogo 143,053 (wanaume 57,221 na wanawake 85,832) kusajiliwa kwa hiari yao tangu zoezi lilipoanza Machi 2024.

55. ***Mheshimiwa Spika***, kati yao, wafanyabiashara 63,246 (Wanaume 24,965 na Wanawake 38,281) wamelipia gharama za uchapishaji wa vitambulisho vya kidijitali. Aidha, wafanyabiashara 51,333 sawa na asilimia 81.2 ya waliolipia tayari wamepatiwa vitambulisho vyao, huku maombi 11,913 sawa na asilimia 18.8 yapo katika hatua za uchapishaji na usambazaji. Vitambulisho hivi vinachapishwa na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC) kilichopo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambacho kina mkataba na Wizara wa kutekeleza jukumu hilo. Kituo hicho ni maalum kwa ajili ya kuchakata na kuhifadhi taarifa mbalimbali kidijitali.

56. ***Mheshimiwa Spika***, kitambulisho cha kidijitali cha wafanyabiashara ndogondogo ni muhimu kwa kuwa, hubeba taarifa za msingi kama vile taarifa za biashara, eneo la biashara na shughuli za kiuchumi za mhusika tofauti na kitambulisho cha NIDA ambacho kina taarifa

binafsi za mhusika ikiwemo uraia wake. Mfumo huo unawawezesha wafanyabiashara hao kutambulika rasmi na kurahisisha upatikanaji wa mikopo, huduma za kifedha, masoko na fursa nyingine za uwezeshaji wa kiuchumi.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kitambulisho hicho kimeunganishwa na mifumo mingine kama vile NIDA, mifumo ya hifadhi ya jamii, mifumo ya kibenki na Wezesha Portal ambapo muunganiko huo umewezesha kusomana na kubadilishana taarifa za waombaji wa mikopo hiyo.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mafunzo kuhusu Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa wafanyabiashara ndogondogo (Wafanyabiashara Ndogondogo *Management Information System - WBN-MIS)* kwa washiriki 139 ambao ni maafisa wa Serikali kutoka ngazi ya Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Viongozi wa Wafanyabiashara Ndogondogo. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha uratibu, usimamizi na utekelezaji wa zoezi la utambuzi na usajili wa wafanyabiashara ndogondogo nchini.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo. Fedha hizo

zinafanya jumla ya shilingi bilioni 18.5 zilizopokelewa na Wizara na kupelekwa Benki ya NMB kwa ajili ya utoaji wa mikopo tangu zoezi hilo lianze mwezi Januari, 2025. Aidha, hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 8,426 (Wanaume 3,906 Wanawake 4,520) wamekopeshwa kiasi cha shilingi bilioni 17.9. Mchanganuo wa Mikopo hiyo kwa kila Mkoa umeambatishwa katika ***Kiambatisho Na.1.***

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI pamoja na Viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) iliratibu makongamano na mikutano ya Wafanyabiashara Ndogondogo katika Mikoa yote 26 kuanzia mwezi Agosti, 2025 hadi Aprili, 2026, ambapo jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 25,458 (Wanaume 10,184 na Wanawake 15,274) walishiriki. Kupitia makongamano na mikutano hiyo, washiriki walipata elimu ya biashara, kujadili mafanikio na changamoto zinazowakabili pamoja na kuunganishwa na fursa zinazotolewa na Taasisi mbalimbali. Taasisi zilizoshiriki ni pamoja na Benki ya NMB, CRDB, Benki ya Azania, TRA, SIDO, TANESCO, NSSF, Tanzania Agricultural Development Bank – TADB na NHIF.

61. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Sekta nyingine hutoa nafasi za ushiriki wa wafanyabiashara ndogondogo katika maonesho ya biashara za ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI, iliratibu ushiriki wa wafanyabiashara ndogondogo 1,374 (Wanaume 632 na Wanawake 742) katika Maonesho ya Kitaifa ya Wakulima na Wafugaji (Nanenane) mwezi Agosti, 2025 yaliyofanyika Jijini Dodoma ambapo waliweza kuuza na kutangaza biashara zao. Aidha, jumla wafanyabishara ndogondogo 697 (Wanaume 237 na Wanawake 460) walitembelea banda la Wizara na kuelimishwa kuhusu fursa ya mikopo yenye masharti nafuu inayoratibiwa na Wizara kupitia Benki ya NMB.

62. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na OWM – Kazi, Ajira na Mahusiano pamoja na Wizara nyingine za Kisekta iliwawezesha wafanyabiashara 271 (Wanaume 122 na Wanawake 149) kushiriki katika Maonesho ya 25 ya wajasiriamali wadogo na wa kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Juakali/Nguvukazi) yaliyofanyika Jijini Nairobi – Kenya mwezi Novemba 2025. Kupitia Maonesho hayo wafanyabiashara hao walipata fursa ya kuonesha na kuuza bidhaa

zao, kupata uzoefu kutoka kwa wenzao na hatimaye kukuza mtandao wa kibiashara.

63. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Umoja wa Mamalishe na babalishe Tanzania (UMALITA), OWM - TAMISEMI, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na sekta binafsi, iliandaa Kongamano la Kitaifa lilishirikisha mamalishe na babalishe 3,500 kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, lililofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 21 Aprili 2026. Pamoja na masuala mengine, kongamano hilo lililenga kuimarisha nafasi ya mamalishe na babalishe katika uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla kwa kuwaunganisha, kuwajengea uelewa na kuwawezesha kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo katika mnyororo wa thamani wa chakula.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** kongamano hilo pia lililenga kuweka msingi wa kuwawezesha wafanyabiashara hao kushiriki kikamilifu katika uchumi rasmi kupitia mafunzo, teknolojia, masoko, mitaji na matumizi ya nishati safi, ili kujenga uchumi jumuishi, shindani na unaozalisha ajira kwa wananchi wengi zaidi. Vilevile, kongamano hilo lilisisitiza umuhimu wa kuwaandaa mamalishe na babalishe kunufaika na fursa za kiuchumi zitokanazo na

matukio mbalimbali makubwa ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo **AFCON 2027**, hususan katika huduma za chakula, utalii, biashara na huduma nyingine zitakazochochea ongezeko la kipato na ukuaji wa biashara zao. **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa Mgeni Rasmi katika tukio hilo kubwa. Kongamano liliongozwa na kauli mbiu isemayo ***"Shiriki Kulinda Amani na Mshikamano wa Taifa; Amani ni Hazina Yetu, Mamalishe na Babalishe".***

65. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa mikopo pamoja na elimu ya fedha na ujasiriamali kwa wafanyabiashara ndogondogo kupitia Benki za Biashara nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya wafanyabiashara ndogondogo **60,737** (Wanaume 42,137 na Wanawake 18,600) wamenufaika na mikopo yenye thamani ya **Shilingi trilioni 1.8**. Kati ya Fedha hizo, Wanaume walipata mikopo yenye thamani ya **shilingi trilioni 1.357**, sawa **na asilimia 75.4** na wanawake walipata mikopo yenye thamani ya **Shilingi trilioni 0.443**, sawa na **asilimia 24.6**. Hatua hii imeendelea kuchochea ukuaji wa biashara ndogondogo nchini, kuongeza ujumuishwaji kifedha na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uchumi rasmi.

66. ***Mheshimiwa Spika***, huduma za mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo zinaendelea kutolewa kupitia programu mbalimbali za benki za biashara nchini. Programu hizo ni pamoja na mikopo ya kilimo na biashara kupitia Benki ya NMB; Mikopo ya wajasiriamali wadogo kupitia benki ya kupitia Benki ya *Equity;* mikopo ya mtu mmoja mmoja na vikundi kupitia Benki ya TCB*;* Mikopo ya Kua Nasi kupitia Benki ya NBC; na Mikopo ya IMBEJU kupitia *CRDB Foundation*.

67. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Benki ya Azania inaendelea kutoa mikopo ya Fanikisha Wewe ni Hodari, mikopo ya viwanda skimu na mikopo ya biashara ndogondogo. Aidha, Benki ya *DCB* inatoa Mikopo ya Tausi, Sokoni, mikopo ya bajaji na bodaboda huku Benki ya Maendeleo ikitoa mikopo ya Wezesha Machinga, mikopo ya vikundi (Solidarity Group Lending - SGL) na mikopo ya Bajaji kwa kushirikiana na Chama Cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (CMPD).

## ENEO LA 4: MALEZI, MAADILI, MAENDELEO NA USTAWI WA WATOTO

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia malezi, maadili, matunzo na ustawi wa watoto pamoja na familia, ambayo ni msingi wa kujenga Taifa

lenye nguvukazi yenye tija. Malezi chanya ya watoto yanayoambatana na maadili mema ni nguzo katika kujenga Taifa imara kwa ustawi na maendeleo endelevu. Sambamba na hilo, Wizara inaratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya malezi chanya kwa wazazi au walezi na vijana balehe, ikiwa ni juhudi za pamoja za kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** watoto ni rasilimali muhimu na mtaji wa Taifa, hivyo wanapaswa kulindwa, kupendwa, kuendelezwa na kulelewa katika misingi ya maadili na tamaduni za Taifa letu, ambapo mazingira bora na sahihi ya malezi ya watoto yanapaswa kuanzia ndani ya familia. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo hali duni ya kipato cha familia, ukatili, migogoro ya familia, na vifo vya wazazi au walezi, husababisha watoto kuishi katika mazingira hatarishi hivyo kuhitaji huduma za malezi mbadala.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22–2025/26). Programu hiyo inalenga kuhakikisha kuwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka nane (8) anapata huduma jumuishi za malezi na makuzi ili kuongeza kiwango cha

ukuaji timilifu kutoka asilimia 47 ya sasa hadi asilimia 90 kama ilivyobainishwa katika DIRA 2050. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara imeratibu uandaaji wa mfumo wa upimaji wa matokeo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (Early Childhood Development – ECD Scorecard) ili kufuatilia utekelezaji wa viashiria vya Programu hiyo.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa mfumo kwa ajili ya kukusanya takwimu na taarifa kuhusu afua za malezi na makuzi ya awali ya mtoto kutoka katika mifumo ya Wizara za kisekta na Taasisi mbalimbali za Serikali (ECD Dashboard). Mfumo huo unalenga kubaini ulinganifu wa utekelezaji wa nguzo tano (5) za Malezi na Makuzi ya watoto wadogo ambazo ni afya bora, lishe toshelevu, uchangamshi na ujifunzaji wa awali; malezi yenye mwitikio; na ulinzi na usalama wa watoto wadogo. Nguzo hizo zote zina umuhimu sawa katika malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wadogo. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kuhusu mifumo hiyo kwa maafisa wasimamizi 227 kutoka Mikoa na Halmashauri zote nchini. Kati yao, maafisa 17 walitoka ngazi ya Wizara, maafisa 26 kutoka ngazi ya Mkoa, na maafisa 184 kutoka ngazi ya Halmashauri.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya vifaa vya kielektroniki kwa watoto, hali inayochangia upatikanaji wa maudhui yasiyofaa kwa watoto. Tafiti zinaonesha kuwa asilimia 67 ya watoto wenye umri wa miaka 12–17 hutumia simu janja, ambapo asilimia 4 kati yao wamekumbana na aina mbalimbali za ukatili mtandaoni. Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto dhidi ya changamoto hizo, Wizara ilitoa mafunzo kwa timu ya wawezeshaji 516 kuhusu usalama wa watoto mtandaoni, kwa lengo la kuwawezesha kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu na watumishi wasio walimu katika shule za msingi na sekondari. Baada ya mafunzo hayo, wawezeshaji waliweza kuwaelimisha wanafunzi 1,811,212, walimu 679 na watumishi wasio walimu 232 kutoka mikoa yote 26 nchini.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Serikali inaendana na kasi ya maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ilianzisha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Usalama wa Mtoto Mtandaoni mwaka 2024 kwa lengo la kuishauri Wizara kuhusu afua mahsusi zinazokidhi mahitaji ya wakati wa sasa. Kamati hiyo hukutana kila robo mwaka. Moja ya ushauri uliotolewa na Kamati ni uwezekano wa matumizi ya utaratibu maalum wa kuchuja na kuzuia maudhui yasiyofaa kwa

watoto wanapotumia mitandao. Sambamba na hilo, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ipo katika hatua ya majadiliano ya kuanzisha matumizi ya Laini Maalum ya Simu kwa Mtoto (Child SimCard) kwa lengo la kuimarisha usalama wa mtoto katika matumizi ya teknolojia na mawasiliano.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za kundi la vijana balehe ikiwemo maambukizi ya VVU na UKIMWI, mimba za utotoni, vitendo vya ukatili, lishe duni, watoto kuacha shule, pamoja na ukosefu wa ujuzi na fursa za kiuchumi, Wizara imeratibu utekelezaji wa Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (2021/2022 – 2024/2025). Katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ilifanya tathmini ya utekelezaji wake, na imependekezwa kuanzishwa kwa Programu Jumuishi ya Taifa inayolenga kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe wenye umri wa miaka 9 hadi 19.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinavyoathiri afya ya mwili na akili. jumla ya walimu 4,388

wamepata mafunzo kuhusu namna ya kuanzisha, kusimamia na kuratibu afua za ulinzi na usalama wa mtoto shuleni. Aidha, Wizara imeanzisha na kuimarisha madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari nchini. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Madawati 3,204 ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto yameanzishwa katika shule za msingi na sekondari nchini na hivyo kufikisha jumla ya madawati 11,156 kati ya lengo la madawati 20,772 ifikapo mwaka 2027/28.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara imeratibu na kusimamia uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto kwa lengo la kuwapa watoto fursa ya kushiriki katika mijadala ya masuala yanayowahusu kulingana na umri wao. Katika kipindi hicho, mabaraza 223 yalianzishwa na kufanya jumla ya mabaraza kufikia 8,427 kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa. Hata hivyo, Wizara inaendelea na jitihada za kuanzisha mabaraza kwenye vijiji/Mitaa ili kufikia azma ya Serikali ya kuwa na mabaraza 16,602 ifikapo 2027/28.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na vitendo vya ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto wa kike ambavyo ni ukiukwaji wa haki za binadamu, Serikali imezindua Mkakati wa Taifa wa Kisekta wa Kutokomeza Ukeketaji

(2025/26 – 2029/30), unaolenga kuimarisha juhudi za kutokomeza vitendo vya ukeketaji nchini. Mkakati huo unalenga kupunguza kiwango cha ukeketaji kutoka asilimia 8 hadi kufikia asilimia 4 ifikapo mwaka 2030. Tofauti na mikakati iliyopita, mkakati huu umeweka kipaumbele cha ushiriki wa wanaume katika harakati za kutokomeza ukeketaji. Hatua hiyo inatokana na baadhi ya mila, desturi na mitazamo hasi ya jamii inayochochea vitendo vya ukeketaji hususani kwa baadhi ya wanaume kutokuwa tayari kuoa wanawake ambao hawajakeketwa

78. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hatua hiyo, kwa mwaka 2026 Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji katika Mikoa yenye vitendo vya ukeketaji nchini. Aidha, Wizara iliungana na Mkoa wa Arusha katika Maadhimisho ya kupinga vitendo vya ukeketaji yaliyofanyika mwezi Februari, 2026 katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Katika maadhimisho hayo jumla ya wananchi 3,227 walipata elimu kuhusu madhara ya ukeketaji na umuhimu wa ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za kuelimisha jamii.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu afua za ulinzi na usalama wa watoto wanaokinzana na kukutana na sheria pamoja

na watoto walio katika mazingira hatarishi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya watoto 284,308 (Wavulana 183,124 na Wasichana 101,184) walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani na watoto waliokinzana na sheria wametambuliwa na kupatiwa afua mbalimbali za kiustawi ikiwemo malezi mbadala, elimu, mafunzo ya ufundi stadi, huduma za afya, vifaa vya shule na kuwaunganisha na familia zao.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani wamegawanyika katika makundi mawili, wanaotegemea mtaa kama makazi ya kudumu na wanaofanya kazi mtaani na kurudi kwenye familia ya wazazi au walezi wao. Katika kipindi husika Wizara imeendesha Kampeni rafiki ya kuokoa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani katika mikoa yote nchini. Kupitia kampeni hiyo, jumla ya watoto 6,182 (Wavulana 3,407 na Wasichana 2,775) wameokolewa, watoto 5,663 wameunganishwa na familia zao, kati yao watoto 52 wamehitimu mafunzo mbalimbali ya ufundi, 448 wako katika Makao ya Watoto na 71 wako chini ya walezi wa kuaminika.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuzuia watoto kuingia mtaani, Sambamba na hilo, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana

na OWM - TAMISEMI imeanzisha Madawati 14 ya huduma za Ustawi wa Jamii katika Bandari ya Dar es Salaam na stendi za mabasi katika Mikoa ya Shinyanga (2), Mwanza (2), Dar es Salaam (2), Arusha, Kagera, Mbeya, Morogoro, Dodoma, Njombe, Tabora na Ruvuma. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya watoto 3,366 (Wavulana 1,679 na Wasichana 1,687) wameokolewa kupitia madawati hayo na kuunganishwa na familia na wengine kupata huduma katika makao ya watoto.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** madawati hayo hutumika pia kutoa huduma za Ustawi wa Jamii kwa watu wazima wenye changamoto mbalimbali ikiwemo waliopotezana na ndugu zao, waliokosa nauli, waliotelekezwa, waliotapeliwa na waliopitia kadhia ya usafirishaji haramu wa binadamu. Jumla ya watu wazima 3,139 (Wanaume 1,672 na Wanawake 1,467) wamepatiwa huduma katika madawati hayo. Afua hizi zinatekelezwa kupitia Kiongozi cha Uratibu, Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii cha mwaka 2025.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasisitiza kwamba, watoto wote walelewe katika familia. Wazazi na walezi wawajibike katika matunzo na ulinzi wa watoto wao. Mkakati wa kuzuia watoto kuingia na kuishi mtaani ni endelevu ambapo Wizara imepanga kuanzisha madawati

mengine nane (8) katika vituo vya usafirishaji kwenye mikoa mingine, sambamba na kuimarisha uwezo wa watoa huduma, mifumo ya uratibu na ufuatiliaji, pamoja na kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu malezi, makuzi na ulinzi wa watoto.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, inapotokea watoto wamekosa malezi ya kifamilia, Wizara imeweka utaratibu wa malezi mbadala kama vile huduma za watoto wanaolelewa katika Makao ya Watoto, Malezi ya Kambo na Kuasili kwa lengo la kutoa matunzo kwa watoto hao. Katika kipindi husika jumla ya Makao ya Watoto 33 yanayomilikiwa na kuendeshwa na Taasisi Binafsi yamesajiliwa na kufanya kuwa na jumla ya makao 426 yaliyosajiliwa nchini (Serikali 2 na Binafsi 424). Makao hayo yanahudumia jumla ya watoto 16,648 (Wavulana 8,423 na Wasichana 8,225).

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji, jumla watoto 39 (Wavulana 18 na Wasichana 21) wamepatiwa huduma ya malezi ya kambo na jumla watoto 28 (Wavulana 11 na Wasichana 17) wamepatiwa huduma ya malezi ya kuasili. Wito unatolewa kwa wote wenye mapenzi mema na watoto na wanaohitaji huduma za kutoa malezi ya kambo na kuasili watoto wafanye maombi yao kupitia Afisa

Ustawi wa Jamii kwenye eneo lao kwa hatua stahiki.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa mfano kwa kuendesha Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo - Dodoma na Kurasini - Dar es Salaam yanayotoa huduma jumuishi kwa watoto. Huduma hizo ni pamoja na mahitaji ya msingi, afya, unasihi, elimu ya awali, mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya ujasiriamali, kilimo, ufugaji na kuwaunganisha watoto na familia. Jumla ya watoto 418 (Wavulana 231 na Wasichana 187) wamehudumiwa; ambapo Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo yamehudumia watoto 229 (Wavulana 119 na Wasichana 110) na Makao ya Watoto Kurasini yamehudumia watoto 189 (Wavulana 112 na Wasichana 77). Kati ya hao, jumla ya watoto 90 (Wavulana 49 na Wasichana 41) wameunganishwa na familia zao au familia mbadala.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Katiba na Sheria imefanya usimamizi shirikishi kuhusu utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya utoaji huduma za Ustawi wa Jamii katika makao ya watoto katika Mkoa wa Dar es Salaam na Arusha. Zoezi hilo limefanyika kwa kutembelea makao ya watoto 25 katika Mkoa wa Dar es Salaam na Makao ya watoto tisa (9)

katika Mkoa wa Arusha. Kupitia zoezi hilo wamiliki wa makao ya watoto 34 pamoja na maafisa ustawi wa jamii 85 walijengewa uwezo wa kuandaa mipango ya huduma kwa watoto.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha haki, ulinzi na ustawi wa watoto kupitia mfumo wa sheria na kijamii, Serikali imeweka mazingira rafiki yanayowezesha watoto waliokinzana au kukutana na sheria kusikilizwa katika Mahakama za Watoto, kwa kuzingatia maslahi mapana ya mtoto na haki zake za msingi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya mashauri 1,367 (Wavulana 731 na Wasichana 636) yalisikilizwa katika Mahakama za Watoto. Kati ya mashauri hayo, mashauri 1,248 ni ya madai na mashauri 119 ni ya jinai. Kati ya mashauri ya madai yaliyosikilizwa, mashauri 1,231 yalihusu matunzo ya watoto, uangalizi wa watoto, haki ya kuwaona watoto pamoja na kuasili watoto na mashauri 17 yalihusu vipimo vya vinasaba.

89. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa huduma za haki za mtoto Kisheria na Marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria katika Mahabusu za Watoto 6 nchini (Arusha, Mbeya, Tanga, Moshi, Upanga – Dar es Salaam na Mtwara) na shule ya Maadilisho ya Irambo Mkoani Mbeya ambapo jumla ya watoto 154 (Wavulana 148 na Wasichana 6)

wamepatiwa huduma za msingi ikiwemo chakula, malazi, mavazi, afya, stadi za maisha, msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa lengo la kuwezesha marekebisho ya tabia na utengamao. Huduma hizo zimewezesha watoto kurekebishwa tabia na kupata stadi za maisha za kuwasaidia kujitegemea.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kuimarisha afua zinazolenga kuwaandaa vijana kuingia katika majukumu ya ndoa na familia. Kadhalika, Wizara imeweka msisitizo wa umuhimu wa utatuzi wa migogoro ya familia kwa njia ya usuluhishi ambapo, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imepokea jumla ya mashauri ya ndoa 49,573. Kati ya mashauri hayo, mashauri 9,995 yamesuluhishwa na kufungwa, mashauri 8,036 yalipelekwa mahakamani na mashauri 31,542 yanaendelea kusuluhishwa.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya mashauri ya matunzo ya watoto 19,425 yalitokana na watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Kati ya mashauri hayo 3,500 yamepelekwa Mahakamani na mashauri 15,925 yanaendelea kushughulikiwa na Maafisa Ustawi wa Jamii. Juhudi za kushughulikia migogoro ya familia na ndoa zinachangia kuimarisha mahusiano, ustawi wa familia, na kuwezesha wahusika kushiriki

kikamilifu katika shughuli za maendeleo pindi changamoto zao zinapotatuliwa.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, Wizara inasajili vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana 922 vimesajiliwa na kufikia jumla ya vituo 4,916 kote nchini vinavyohudumia jumla ya Watoto 565,508 (Wavulana 267,922 na Wasichana 297,586). Vilevile, jumla ya Vituo 282 vya Malezi ya Watoto vya Kijamii vimeanzishwa katika ngazi ya jamii vilivyotoa huduma kwa watoto 23,137 (Wavulana 9,875 na Wasichana 13,262). Uwepo wa vituo hivyo umesaidia malezi na matunzo ya awali ya watoto na kuwezesha wazazi kupata muda wa kujishughulisha na shughuli za kiuchumi.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuimarisha usajili na ufuatiliaji wa vituo hivyo ili kuhakikisha vinazingatia viwango na miongozo iliyowekwa; kujenga uwezo wa watoa huduma kupitia mafunzo ya malezi, lishe na ulinzi wa mtoto; pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na jamii katika uwekezaji wa huduma za malezi ya awali.

94. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau wake wa kisekta imeendelea kuratibu ushirikiano wa wadau mbalimbali wa maendeleo ili kushirikiana na jamii ya makundi yote katika kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa watoto ambapo, kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi, idadi ya watoto walioripotiwa kufanyiwa ukatili wa kingono imepungua kutoka 10,937 mwaka 2024 hadi 9,902 kwa mwaka 2025 (Mchanganuo wa takwimu husika kwa watoto wa kike na kiume na kwa aina ya matukio upo kwenye ***Kiambatisho Na.2A***). Hata hivyo, pamoja na mafanikio haya, takwimu hizi zinaonesha ukubwa wa changamoto ya ukatili dhidi ya watoto katika jamii yetu na zinatoa wito kwa Taifa kuendelea kuchukua hatua madhubuti zaidi za kulinda kizazi cha sasa na kijacho hivyo, Wizara itaendelea kwa kasi zaidi kuratibu wadau wake ili kuhakikisha ukatili wa kingono dhidi ya watoto unatokomezwa.

95. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, watoto wameendelea kukabiliwa na ukatili wa kutupwa, kuibwa na kutelekezwa ambapo, kwa mwaka 2025 taarifa ya Jeshi la Polisi inaonesha kwenye ***Kiambatisho Na.2B*** kuwa, jumla ya watoto 165 waliripotiwa kutupwa, 137 kutelekezwa na 86 kuibwa. Matukio haya

ni kinyume na haki za watoto kuishi kama ilivyoainishwa katika sera ya maendeleo ya mtoto na sheria ya mtoto. Wizara kwa kuunganisha nguvu na wadau wake itaendelea kuelimisha jamii kuimarisha ulinzi wa watoto na iwapo kuna mzazi wa mwenye changamoto yoyote, taarifa iwasilishwe ustawi wa jamii ili hatua zinazostahili zichukuliwe ikiwemo kutoa huduma ya malezi mbadala na kwa wale wenye uhitaji wa watoto badala ya kuwaiba wafahamu kuhusu uwepo wa huduma rasmi ya kisheria ya kuasili watoto. Tofauti na mwelekeo huu Serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wote wanaojihusisha na vitendo vya ukatili na kuhujumu haki za watoto.

96. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha haki za watoto zinalindwa, wizara kupitia maafisa ustawi wa jamii imeendelea kufuatilia mashauri ya kesi mbalimbali mahakamani ambapo, wakati tunaanza mwaka wa fedha Julai 2025 kulikuwa na mashauri 1,237 ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto yaliyokuwa yanaendelea Mahakamani. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2025 hadi 30 Aprili, 2026 mashauri mapya 1,909 yaliwasilishwa Mahakamani, hivyo kufanya jumla ya mashauri ya ukatili dhidi ya watoto yaliyofikishwa Mahakamani kufikia **3,146**. Kati ya mashauri hayo,

mashauri **2,517** yamekwishapatiwa maamuzi huku mashauri **629** yakiendelea kusikilizwa Mahakamani.

97. ***Mheshimiwa Spika***, ni ukweli usiopingika kuwa, Taifa lenye maono ya kufikia DIRA ya Taifa ya Maendeleo 2050 haliwezi kujengwa juu ya mazingira yanayoruhusu watoto kuishi katika hofu, manyanyaso na kukosa ulinzi stahiki hivyo, tunapoelekea DIRA 2050 ni lazima tutambue kuwa, msingi wa Taifa imara, lenye uchumi shindani na maendeleo endelevu ni uwekezaji katika malezi bora, usalama na ustawi wa watoto.

98. ***Mheshimiwa Spika***, ijulikane kwetu sote kuwa, mapambano dhidi ya ukatili wa watoto si jukumu la Serikali pekee bali ni wajibu wa Taifa nzima hivyo, tunapaswa kama jamii kuungana kwa dhati wazazi, walezi, viongozi wa dini, viongozi wa mila, walimu, vyombo vya dola na wananchi wote kuhakikisha watoto wanalelewa katika mazingira salama, yenye maadili, upendo na heshima kwa utu wa binadamu kwani, bila kufanya hivyo, tutakuwa tunahatarisha msingi wa kizazi chenye jukumu la kubeba maono, uchumi na uongozi wa Tanzania ya mwaka 2050.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wazazi wanatekeleza wajibu wao wa kusimamia maadili, malezi na matunzo ya watoto na familia, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu kuhusu maadili, malezi chanya na matunzo ya watoto na familia, yenye kaulimbiu isemayo "**Familia Bora, Taifa Imara.**" Katika kipindi husika, jumla ya wazazi na walezi 469,634 (Wanaume 157,291 na Wanawake 312,343) walipatiwa elimu ya malezi chanya kupitia majukwaa ya wazazi, viongozi wa dini na wahamasishaji jamii. Sambamba na hilo, elimu hiyo ilitolewa kwa waandishi wa habari kutoka vyombo vya habari 29 vya Kitaifa pamoja na redio za kijamii 16 zinazosikika nchi nzima.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** vikundi vya malezi ni majukwaa ya kuwafikia wazazi na walezi kwa urahisi katika lengo la kuimarisha malezi, matunzo na maadili ya watoto ndani ya familia. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeandaa Mwongozo wa kuwezesha uanzishaji na uendeshaji wa Vikundi vya Malezi na Matunzo ya Watoto. Katika kipindi husika, jumla ya vikundi vya malezi 4,526 vimeanzishwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Lengo la Serikali ni kuanzisha na kuhuisha vikundi 200,000 vya malezi na

matunzo ya watoto ifikapo mwaka 2030. Hatua hiyo ni sehemu ya Makubaliano ya Bogota, Colombia ya mwaka 2024 kuhusu uanzishaji wa majukwaa ya wazazi au walezi kwa ajili ya malezi ya watoto (Bogota Parenting Platforms Agreement, 2024).

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua umuhimu wa ushiriki wa wazazi na walezi katika programu za malezi na matunzo ya watoto nchini. Hata hivyo, imebainika kuwa wazazi wengi hawashiriki ipasavyo katika programu hizo. Kwa kutambua hali hiyo, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) imeratibu utafiti wenye lengo la kubaini tabia na vikwazo vinavyowakabili wazazi na walezi katika kushiriki programu mbalimbali za malezi na matunzo ya watoto.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwa, vikwazo vinavyosababisha wazazi na walezi kutokamilisha programu za malezi ni pamoja na uelewa mdogo wa maudhui ya afua za malezi, umbali wa kufikia maeneo ya huduma hizo, na mwingiliano kati ya shughuli za kiuchumi na muda wa kushiriki programu hizo. Kupitia matokeo hayo, Wizara

inaendelea kuimarisha utekelezaji wa programu za malezi, zikiwemo matumizi ya teknolojia kupitia programu ya malezi kwa njia ya mtandao (Parenting App) ili kuongeza ushiriki wa wazazi na walezi.

## ENEO LA 5: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

103. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa mtu binafsi, familia na makundi mbalimbali katika jamii kwa lengo la kuzuia na kutatua athari zinazotokana na changamoto mbalimbali. Huduma za ustawi wa jamii zinazotolewa kwa makundi hayo zinalenga kukidhi mahitaji ya msingi, kulinda utu wao, na kuwawezesha wanufaika kujenga ustahimilivu wa maisha na hatimaye kujitegemea. Huduma hizo ni pamoja na huduma za msingi za malazi, mavazi, chakula na matibabu; msaada wa kisaikolojia na kijamii; elimu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto; usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia; hifadhi kwa manusura wa vitendo vya ukatili; malezi mbadala; marekebisho ya tabia; na kuunganishwa na mifumo mingine ya utoaji huduma ikiwemo huduma za kisheria, afya na uchumi. kwa ujumla, juhudi hizo zinaakisi dhamira ya serikali ya kuhakikisha makundi hayo yanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika uchumi na maendeleo ya taifa.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo inaendelea kutoa huduma za msingi kama vile huduma za matibabu, malazi ya muda, huduma za kisheria na msaada wa kisaikolojia kwa manusura na wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Miongoni mwa vituo vya kutolea huduma hizo ni pamoja na nyumba salama na vituo vya huduma jumuishi vilivyopo katika vituo vya afya. Katika katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya manusura 1,313 (wanaume 53, wanawake 1,260) wamehudumiwa katika nyumba salama 20 zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini. Sambamba na hilo, jumla ya wahanga na manusura wa vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto 108,819 ikijumuisha watoto 32,150 (Wavulana 6,592 na Wasichana 25,558) na watu wazima 76,669 (Wanaume 16,882 na Wanawake 59,787) wameripotiwa katika vituo mbalimbali vinavyotoa huduma za afya kwa manusura wa ukatili nchini.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii kwa lengo la kusogeza huduma za ustawi kwa wananchi ambapo, katika mwaka wa fedha 2025/26 jumla ya Maafisa Ustawi wa Jamii 401 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi, hivyo kufanya idadi yao kufikia 2,315 sawa na asilimia 12.5 ya

Maafisa 18,481 wanaohitajika nchi nzima. Aidha, katika kusogeza huduma za ustawi wa jamii kwa wananchi, Wizara imewapatia Simu Janja Maafisa Ustawi wa Jamii wa ngazi za mikoa ili waweze kuharakisha utoaji wa huduma za kiustawi. Namba za simu kwa kila Mkoa zimeainishwa katika ***Kiambatisho Na.3***.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI, Wizara za kisekta na Wadau wa Maendeleo iliandaa Wiki ya Ustawi wa Jamii yaliyofanyika katika Halmashauri zote nchini kuanzia tarehe 25 - 30 Agosti, 2025 iliyoongozwa na kaulimbiu isemayo **"Pata Msaada wa Kisaikolojia; Imarisha Afya ya Akili"**. Tukio hilo lilitoa fursa kwa wananchi kuzifahamu huduma za ustawi wa jamii sambamba na kufanikisha utolewaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kilele cha Wiki ya Ustawi, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Dar es Salaam ilitoa huduma mbalimbali zikiwemo: - Usajili wa Vituo vya kulelea Watoto Wadogo mchana (122); Kutolewa kwa Vyeti vya Kuzaliwa (53); Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa (86); Uchunguzi wa Afya na matibabu kwa wananchi (62); Uchunguzi wa Afya ya Ngozi na Matibabu kwa Watu Wenye Ualbino (263); Kutolewa kwa Huduma ya Msaada wa Kisheria kwa Wananchi (117).

Aidha, Wananchi (83) walijiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Wananchi (117) Walipatiwa Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Watoto (43) wanaoishi na kufanya kazi Mtaani waliunganishwa na familia zao; na Manusura (22) wa vitendo vya ukatili walipatiwa usaidizi wa haraka wa huduma za kisaikolojia, Afya na kisheria. Huduma hizo pia zilitolewa katika Halmashauri na Mikoa yote nchini.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO, Tanzania STEPS Survey - 2023) ulionesha kuwa, takribani watu 25 kati ya watu 100 hukabiliwa na changamoto za afya ya akili na saikolojia. Takwimu hizi zinaonesha wazi kuwa changamoto za afya ya akili si suala la mtu mmoja mmoja, bali ni suala linalohitaji juhudi za pamoja. Katika kipindi cha mwezi Julai 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya Wataalam 95 wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii, Madaktari na Wauguzi wanaotoa huduma kwa Watoto na Vijana balehe kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Kagera na Songwe wamejengewa uwezo juu ya kutoa huduma ya Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii (Mental Health and Psychosocial Support – MHPSS).

109. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, watoa huduma ngazi ya jamii 280 wamejengewa uwezo wa utoaji wa huduma ya msaada wa afya ya akili na msaada wa kisaikolojia wakati wa majanga katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Katavi, Kigoma, Dodoma, Mbeya na Dar es Salaam. Aidha, wahudumiwa 490 (Wanaume 286 na Wanawake 204) katika vituo vya Ustawi wa Jamii wamepata huduma ya Afya ya Akili na Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii. Pia, jumla ya watoto 208,921 (Wavulana 99,744 na Wasichana 109,177) walio katika mazingira hatarishi na jumla wa wananchi 99,136 (Wanaume 49,568 na Wanawake 49,568) wamepata huduma hiyo. Mafunzo haya yameimarisha uwezo wa wataalam kutambua mapema changamoto za afya ya akili kwa watoto na vijana, kutoa huduma stahiki za ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia, pamoja na kushughulikia athari za msongo wa mawazo, ukatili na majanga mbalimbali.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuimarisha utolewaji wa huduma za Ustawi wa Jamii nchini kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kuongeza ubora wa huduma hizo kwa jamii. Katika kufanikisha hilo, Wizara inashughulikia uanzishwaji wa Idara Huru Inayojitegemea ya Ustawi wa Jamii ambapo kwa sasa iko kwenye hatua ya kupokea maoni kutoka Wizara za

Kisekta. Hatua hii inakwenda sambamba na kukamilisha mchakato wa utungwaji wa sheria mahsusi ya wataalam wa huduma za ustawi wa jamii yenye lengo la kusimamia, kudhibiti maadili na weledi kwa wataalamu wanaotoa huduma za ustawi wa jamii.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua na kuthamini mchango wa Wazee kama Tunu muhimu ya Taifa. Dhamira hiyo imeainishwa katika Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024, inayosisitiza kuhusu ulinzi, matunzo, hifadhi ya jamii na ustawi wa wazee. Taifa lisilojali wazee linapoteza hazina ya maarifa, uzoefu, historia na utamaduni ambavyo ni msingi wa kujenga mshikamano na maadili ya jamii.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026 Wizara imetoa huduma za matunzo kwa wazee na wasiojiweza 229 (Wanaume 139 na Wanawake 90) katika makazi ya Wazee 13 yanayosimamiwa na Wizara. Makazi hayo yapo katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Nunge - Dar es Salaam, Kibiriz - Kigoma, Njoro - Kilimanjaro, Ipuli - Tabora, Kolandoto - Shinyanga, Bukumbi - Mwanza, Magugu - Manyara, Kilima-Kagera, Nyabange - Mara na Mwanzange na Misufini Mkoani Tanga. Sambamba na hilo, Wizara imeratibu huduma za utoaji wa matunzo kwa jumla ya wazee 268 (Wanaume 218 na Wanawake 50)

kwenye Makazi ya Wazee 16 yanayomilikiwa na Taasisi Binafsi.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za afya kwa Wazee nchini ikiwa ni utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imewezesha upatikanaji wa Bima za Afya kwa Wazee wote 229 (Wanaume 139 na Wanawake 90) wanaohudumiwa katika Makazi 13 ya Serikali. Kadhalika, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI imefanikisha upatikanaji wa huduma za Msamaha wa Matibabu na Upimaji wa afya kwa Wazee 586,638 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.2.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee, jumla ya madirisha 1,066 ya kutolea huduma za afya kwa wazee yameanzishwa katika hospitali 187 na vituo vya afya 879 katika Halmashauri 184. Sambamba na hilo, jumla ya Watoa Huduma za Afya 140 katika ngazi ya msingi pamoja na Waandishi wa Habari 20 kutoka vyombo mbalimbali vya habari wamejengewa uwezo juu ya afua zinazohusu huduma na ustawi wa wazee. Pia, Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Help Age Tanzania imeendelea kutoa elimu na

hamasa kuhusu umuhimu wa mazoezi kwa wazee nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya Klabu 195 za mazoezi ya Wazee zimeanzishwa na kupatiwa vifaa vya mazoezi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Morogoro, Kigoma na Shinyanga.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imeratibu uanzishaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee, ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya mabaraza 20,768 yameanzishwa kuanzia ngazi ya Kata hadi Taifa. Mabaraza hayo yanatumika kama majukwaa ya kuwakutanisha wazee na kujadili masuala yanayo wahusu na nafasi yao katika jamii ikiwa ni pamoja na kurithisha mila, tamaduni na maarifa chanya kwa watoto na vijana. Sambamba na hilo, Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida, Simiyu, Mbeya na Morogoro imeanzisha Ofisi za Mabaraza ya Ushauri wa Wazee ambayo yamerahisisha uratibu wa shughuli za mabaraza hayo.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Aprili, 2026, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) imefanya utambuzi wa jumla ya wazee 1,014,005 wenye uhitaji na kuwajumuisha katika mpango wa uwezeshaji wa kaya maskini utakaowasaidia kuboresha hali zao za kiuchumi kwa ustawi na maendeleo

yao. Hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa hakuna kundi linaachwa nyuma katika mchakato wa maendeleo.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee tarehe 01 Oktoba, 2025 yenye kauli mbiu ya **"Wazee tushiriki uchaguzi kwa Ustawi wa Jamii yetu".** Maadhimisho hayo yalianzia katika ngazi za Mikoa na Wilaya yaliyoambatana na makongamano ya wazee na utoaji wa huduma mbalimbali zikijumuisha huduma za afya na afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii ambapo jumla ya wazee 7,917 walipatiwa huduma hizo. Kilele cha maadhimisho hayo Kitaifa yalifanyika Mkoani Ruvuma na kuhudhuriwa na washiriki 814 (Wanaume 511 na Wanawake 303). Lengo la maadhimisho hayo lilikuwa ni kujenga uelewa kwa jamii kuhusu kuwatunza wazee, kuwashirikisha na kuamsha ari ya jamii katika kujiandaa na uzee mwema.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa wazee umeendelea kuimarika kutokana na jitihada kubwa za Serikali za kuhakikisha wanapata ulinzi na kuishi katika mazingira salama. Kutokana na hatua hizo, matukio ya ukatili na mauaji dhidi ya wazee yameendelea kupungua kwa kiwango kikubwa. Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2024 kuliripotiwa matukio 152

(Wanaume 36, Wanawake 116) ya ukatili na mauaji dhidi ya wazee ikilinganishwa na wazee 101 (Wanaume 26 na Wanawake 75) walioripotiwa kwa mwaka 2025.

## ENEO LA 6: MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE

119. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 yenye lengo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeendelea kuratibu na kutekeleza programu na afua mbalimbali zinazolenga kuimarisha ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika nyanja zote za maendeleo. Programu na afua hizo ni pamoja na Programu ya Kizazi Chenye Usawa, Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama, Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia, Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na Ujumuishwaji wa Masuala ya Jinsia katika Sera, Sheria, Mipango na Bajeti.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Wadau wa Maendeleo imefanikisha utekelezaji wa uandaaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia (*Gender Responsive Budget*) kwa Mwaka 2026/27. Kupitia Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango na

Bajeti (2026/27), ulibainisha Wizara Tisa (9) za mfano ambazo ni kinara wa utekelezaji wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia. Wizara hizo ni pamoja na Wizara ya Afya; Maji; Katiba na Sheria; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Viwanda na Biashara; na Mambo ya Ndani ya Nchi; Mikoa Miwili (2) ya Singida na Geita; na Halmashauri mbili (2) za Chalinze na Tandahimba. Lengo ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali unatoa matokeo chanya na kuimarisha usawa wa kijinsia.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi hili limewezesha Serikali kwa mara ya kwanza kuweza kuandaa tamko la uzingatiaji wa masuala ya kijinsia kwenye mipango na bajeti (Gender Budget Statement) ambayo itawasilishwa katika Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka 2026/27. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa na kuzindua Kitini cha Mafunzo ya Uandaaji wa Bajeti yenye Mrengo wa Kijinsia cha mwaka 2026. Kitini hicho kitatumika kufundishia Maafisa na wadau wote wanaohusika na uandaaji wa bajeti. Aidha, Wizara imewajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge (Kamati za Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Katiba na Sheria na kamati ya Bajeti) kuhusu bajeti

yenye mrengo wa kijinsia na itaendeleza mafunzo haya kwa wadau wote.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuhakikisha bajeti zinaandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia mrengo wa kijinsia, imeshirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la Wanawake - UN WOMEN na Shirika la *Plan International* katika kutoa mafunzo kwa wataalam 486 ikijumuisha wataalam 167 (Wanaume 84, Wanawake 83) wa ngazi ya Wizara, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 319 (Wanaume 174, Wanawake 145). Mafunzo hayo yalishirikisha Wakurugenzi wa Sera na Mipango, Ufuatiliaji na Tathimini na maafisa wa uandaaji wa bajeti, Makatibu Tawala Wasaidizi sehemu ya Mipango na Uratibu (M), Waganga Wakuu (M), Maafisa Elimu (M), Maafisa Ustawi wa Jamii (M) na Maafisa Maendeleo ya Jamii (M) na Maafisa Habari (M).

123. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Kizazi Chenye Usawa (2021/22 - 2025/26), ikiwa ni utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa kiuchumi ambalo **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kinara wa utekelezaji kidunia. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Wizara iliratibu Kongamano lililolenga kuonesha

mafanikio ya programu yaliyojumuisha utekelezaji wa miradi ya kiuchumi iliyotekelezwa na wanawake ikiwemo miradi ya uongezaji wa thamani katika bidhaa mbalimbali na teknolojia zinazorahisisha uzalishaji. Kongamano hilo lilishirikisha Waratibu 280 kutoka Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

124. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha mafanikio ya Programu hiyo yanafahamika na kuenezwa kwa umma, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini wa Wizara, Taasisi za Umma na Sekretarieti za Mikoa wapatao 63, pamoja na Wahariri 30 kutoka vyombo mbalimbali vya habari vya Umma na binafsi. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uelewa wanahabari na wahariri kuhusu utekelezaji na mafanikio ya Programu kwenye nyanja mbalimbali.

125. ***Mheshimiwa Spika***, mafunzo hayo yamewezesha wanahabari kuibua, kujadili na kuandaa makala katika vyombo vya habari vya Kitaifa na Kijamii, pamoja na mitandao ya kijamii yakionesha mafanikio yaliyopatikana katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake. Vilevile, Wizara inaendelea na uratibu wa kujenga uelewa kuhusu Programu hii katika ngazi za Mabaraza ya Madiwani, kwa lengo la kujenga uelewa ili waweze kusimamia

utekelezaji wa Programu kwenye maeneo yao, ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 Mabaraza ya Madiwani katika Halmashauri za Chemba, Mpwapwa, Manyoni na Ikungi yamejengewa uelewa.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) imeendelea kuwatumia Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi na Taasisi; ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Kizazi chenye Usawa. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya majiko banifu 13,575, mitungi ya gesi asilia 28,653 na majiko janja ya umeme 7,292 yametolewa kwa wananchi katika Mikoa yote Tanzania bara kwa utaratibu wa ruzuku. Aidha, Taasisi 1,136 zimehamasishwa kutumia nishati safi ya kupikia ikiwemo Taasisi na Vituo vilivyo chini ya Wizara ambazo ni Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Kijitonyama, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii - Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Jamii Ufundi, Makao ya Watoto, Mahabusu za watoto, Shule ya Maadilisho na Makazi ya Wazee.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imewezesha uandaaji wa Mwongozo wa Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika mnyororo wa thamani wa

mazao ya kilimo. Mwongozo huo, unalenga kuziwezesha Taasisi na jamii kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Aidha, sekta ya kilimo imeendelea kuwa kinara katika kuimarisha ushiriki wa wanawake katika ajira zenye staha na shughuli za kilimo chenye tija kupitia uwezeshaji upatikanaji wa ardhi ya kilimo, ushiriki katika mashamba makubwa ya pamoja (BBT Block farms), upatikanaji wa mikopo kwa wanawake (BBT Mitaji) pamoja na kuwawezesha wanawake kuongeza thamani ya mazao.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza muda wa wanawake na wasichana kutafuta maji safi na salama, Serikali imeimarisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya mijini na vijijini. Hali ya upatikanaji wa maji imeongezeka na kufikia **asilimia 85.2** kwa vijijini na **asilimia 92.5** mijini kwa mwezi Desemba, 2026 ikilinganishwa na asilimia 91.6 kwa mijini na asilimia 83 vijijini mwaka 2025.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ushiriki wa wanawake na wasichana kwenye kazi zenye staha, Serikali imeendelea kuhamasiha wasichana kushiriki kwa kusoma masomo ya Sayansi, TEHAMA, Uhandisi na Hisabati kupitia ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wa Programu ya Samia *Scholarship.*

Wanafunzi 936 wamedahiliwa katika mwaka wa masomo 2025/26 ambapo kati ya hao wanawake ni 288 na wanaoendelea na masomo ni wanafunzi 850 ambapo wanawake ni 325 wa shahada ya kwanza na shahada ya uzamili 66 ambapo wanawake ni 24.

130. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund - WDF) unaotoa mikopo kwa Wanawake wajasiriamali walio kwenye vikundi na mwanamke mmoja mmoja. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026, mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 337.9 imetolewa kwa wajasiriamali 45 na kuzalisha jumla ya ajira za watu 114.

131. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wanawake wanafikiwa na fursa za mikopo, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha imeendelea kuhamasisha kutumia madirisha maalum ya wanawake yaliyoanzishwa kwenye Benki mbalimbali nchini. Baadhi ya madirisha hayo ni pamoja na Jasiri Bond (NMB), Malkia Akaunti (CRDB), Fanikiwa Wewe ni Hodari (Azania), Tabasamu (TCB), *Women Suit Loans* (Access Bank Tanzania), *Group and Small* (BRAC Microfinance Tanzania), *Women Entreprenuership Loans* (SELF Microfinance fund), *SME and Micro loans* (Selcom Microfinance Bank), *Women Empowerment Loans* (GADATH Microcredit

Company Limited), *Pink* Mwanamke Loan (Mwanga Hakika Bank), Johari Akaunti (NBC Bank), Vikundi Akaunti (Stanbic bank) na *Mwanamke Plus* (Equity Bank). Kati ya kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026, jumla ya Shilingi **Bilioni 422.9** zimekopeshwa kwa **wanawake 82,699.**

***Natoa rai kwa wanawake wajasiriamali kujiepusha na mikopo yenye masharti magumu ijulikanayo kama mikopo kausha damu, badala yake watumie mikopo iliyopo kwenye utaratibu rasmi unaotambuliwa na Serikali.***

132. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa uundaji na uratibu wa Majukwaa ya Uwezeshaji wanawake Kiuchumi, Toleo la mwaka 2024. Katika kuimarisha majukwaa hayo, Waratibu 26 wa Mikoa na viongozi 130 wa majukwaa ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara walijengewa uwezo kuhusu majukumu na wajibu wao. Vilevile, Sekretarieti ya Kitaifa imeundwa ikiwa na jukumu la kusimamia utekelezaji na kuelimisha fursa za kiuchumi zinazopatikana nchini katika kuwezesha wanawake kiuchumi.

133. ***Mheshimiwa Spika***, wanawake wajasiriamali wameelimishwa kuhusiana na uundaji wa majukwaa na upatikanaji wa fursa za mitaji na mikopo. Jumla ya wanawake 5,096 kutoka Mikoa ya Iringa, Dar es Salaam, Simiyu, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Tanga, Mara, Pwani, Kilimanjaro, Dodoma, Shinyanga, Manyara, Njombe na Songwe walipata elimu hiyo kwa njia mbalimbali ikiwemo kupitia mikutano ya kidijitali.

134. ***Mheshimiwa Spika***, jitihada hizi zimewezesha jumla ya Majukwaa 15,147 kati ya majukwaa 20,748 sawa na asilimia 73 kuhuishwa. Mchanganuo wa majukwaa hayo ni kama ifuatavyo: Ngazi ya Mikoa (Majukwaa 26); Ngazi ya Halmashauri (Majukwaa 184); Ngazi ya Kata (Majukwaa 3,956); Ngazi ya Mitaa (Majukwaa 4,263) na Ngazi ya Vijiji (Majukwaa 6,718).

135. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya ufuatiliaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa na Dodoma. Ufuatiliaji huo ulihusisha kukagua uhai wa vikundi vinavyounda majukwaa, utekelezaji wa shughuli za majukwaa na upatikanaji wa mikopo na mitaji. Kupitia ufuatiliaji huo ilibainika kuongezeka hamasa kwa wanawake kuunda vikundi ili kujiunga na majukwaa. Aidha, majukwaa haya yameendelea

kuwa msaada kwa wanawake kuendelea kukutana na kupata taarifa za fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo fursa za masoko.

136. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha mazingira ya ushiriki wa wanaume katika afua za kukuza usawa wa kijinsia na kupinga ukatili wa kijinsia. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imefanya vikao vilivyohusisha majukwaa ya umoja wa wanaume, ambapo kupitia vikao hivyo kikosi kazi chenye wajumbe sita (6) kiliundwa ili kuunganisha majukwaa hayo kuwa na ushiriki mpana, endelevu na wenye tija. Kutokana na umuhimu huo, Wizara imeanza kuandaa Mwongozo mahsusi wa kuhimiza ushiriki wa wanaume katika kuimarisha usawa wa kijinsia.

137. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imeendelea kuhamasisha vikundi vya wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu kujisajili kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma (National e-Procurement System of Tanzania - NeST) ili waweze kunufaika na zabuni zinazotolewa na Wizara na Taasisi za umma kwa makundi hayo kwa kiwango cha asilimia 30 kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410. Katika kuhakikisha makundi hayo yananufaika, Mafunzo yametolewa kwa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii 978

kutoka Mikoa nane (8) ya Mwanza, Iringa, Mbeya, Songwe, Ruvuma, Katavi, Rukwa na Njombe.

138. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2026 vikundi 1,478 vimepata zabuni za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 39.8, ikijumuisha bilioni 17 zilizonufaisha vikundi vya wanawake 539, bilioni 20.3 kwa vikundi vya vijana 853; bilioni 2.1 kwa vikundi vya Wazee 57 na milioni 295.1 kwa vikundi vya Watu wenye Ulemavu 29. Kupitia zabuni hizo vikundi vimeweza kuongeza uwezo wa kuajiri na kujiajiri, kukuza ujuzi na ushindani wa kufanya kazi za mikataba ya Serikali na kampuni mbalimbali ili kukuza kipato chao.

139. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilifanya Kongamano la Kiuchumi kwa Wanawake na wajasiriamali lililofanyika mwezi Agosti, 2025 Jijini Mbeya lenye Kauli mbiu ya **"Changamkia Fursa: Jenga Leo na Kesho yako".** Kongamano hilo lililohudhuriwa na jumla ya washiriki 3,989 (Wanaume 1,679, Wanawake 2,310). Lengo la Kongamano lilikuwa ni kutoa elimu kuhusu fursa mbalimbali ikiwemo mikopo yenye masharti nafuu, kuwaunganisha na Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, pamoja na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ikiwa pamoja na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) imeendelea kuboresha utendaji wa madawati ya jinsia katika kukabiliana na Ukatili wa Kijinsia, kwa kuandaa mfumo wa kidijitali wa ukusanyaji wa taarifa za Dawati la Jinsia (Gender Desk Information System - GDIS). Mfumo huo utawezesha manusura kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia kwa njia ya faragha. Vilevile, utaimarisha uwezo wa mamlaka kupokea taarifa, kufuatilia na kushughulikia malalamiko kwa wakati na kwa ufanisi.

141. ***Mheshimiwa Spika***, ukatili wa kijinsia ni changamoto inayoathiri uimara wa wanawake na wanaume katika kufikia ndoto zao za kujiletea maendeleo na ustawi. Takwimu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi zinaonesha ukatili wa kingono kwa jinsia zote umeshuka kutoka matukio 12,749 mwaka 2024 hadi 11,625 mwaka 2025. Aidha, katika kipindi chote, wanaokatiliwa zaidi kingono ni wanawake ukilinganisha na wanaume mathalani, wanawake 10,976 na 10,057 walikatiliwa kingono mwaka 2024 na mwaka 2025 mtawalia ukilinganisha na wanaume 1,773 na 1,568 katika kipindi hicho cha

mwaka 2024 na 2025 mtawalia ***Kiambatisho Na.4***.

142. ***Mheshimiwa Spika***, Takwimu za ukatili wa kijinsia kwa watu wazima zinabainisha wazi kuwa, juhudi zaidi zinahitajika katika kuwakomboa wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia kwani, mama akikatiliwa mtoto naye huwa kwenye mashaka makubwa ya kuathiriwa na ukatili huo. Wizara kwa kushirikina na Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Mambo ya Ndani imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuepuka ukatili wa kijinsia, kutumia huduma za dawati la jinsia lililopo katika vituo vyote vya Jeshi la Polisi na kutumia huduma za huduma za msaada wa kisheria chini ya uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria.

143. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, Wizara imeratibu uanzishwaji wa Madawati ya kupinga na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Kati, pamoja na maeneo ya umma yakiwemo maeneo ya masoko. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya madawati 580 yalianzishwa na kufikisha jumla ya madawati 1,150. Mchanganuo wa madawati hayo ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na.2:** Madawati yaliyoanzishwa hadi kufikia Aprili, 2026

| Na. | Eneo | Malengo | Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 | Jumla yaliyoanzishwa hadi Aprili, 2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Taasisi za Elimu ya Juu na Kati | 612 | 30 | 362 | 59 |
| 2 | Maeneo ya soko. | 2,429 | 550 | 788 | 32 |
| | **Jumla** | **3,041** | **580** | **1,150** | **38** |

144. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya Matukio ya ukatili wa kijinsia 150 (41 Maeneo ya masoko na 109 Taasisi ya Elimu ya Juu na Kati) yameripotiwa. Kati ya matukio hayo yaliyoripotiwa, matukio 134 yalipatiwa ufumbuzi. Vilevile, matukio 14 yalitolewa rufaa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na matukio mawili (2) yalipelekwa Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi.

145. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaratibu utekelezaji wa Azimio Na. 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama ambalo Tanzania iliridhia kutekeleza tangu mwaka 2000. Azimio hilo linalenga kuimarisha ulinzi na ushiriki wa wanawake katika ajenda ya

Amani na Usalama kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa. Katika kutekeleza azimio hilo, Wizara, ilizindua Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama (2024/25 - 2028/29) mwezi Agosti, 2025 Jijini Dar es Salaam. Mpango huu unalenga kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki kikamilifu katika kuzuia migogoro, kujenga na kudumisha amani na kushiriki katika mazungumzo ya usalama katika jamii na nchi.

146. ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa Na. 1325, Wizara zote za Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zina umuhimu kutokana na majukumu yao katika kuhakikisha usawa wa kijinsia, amani na ushirikishwaji wa wanawake katika maendeleo na ulinzi wa jamii. Aidha, Wizara 12 za kipaumbele kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ambazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Zanzibar; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum - (Bara); Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - (Zanzibar); Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara nyingine ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Mambo ya Ndani-Jeshi la Polisi; Wizara ya Fedha - Bara; Wizara ya Fedha na Mipango- (Zanzibar); Wizara ya Katiba na Sheria- (Bara); Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora-(Zanzibar); na OWM-TAMISEMI (Bara na Zanzibar). Wizara hizi zimeteuliwa maalum kutokana na uzito wa majukumu yao yanahusiana moja kwa moja na masuala ya usalama, haki, afya, elimu, maendeleo ya jamii, ulinzi wa watoto na wanawake, pamoja na uratibu wa Sera na mipango ya utekelezaji wa Azimio hilo.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huo, Wizara imeratibu vikao kazi vya mashauriano vilivyowashirikisha wataalam 50 wa masuala ya bajeti, ufuatiliaji na tathmini pamoja na watakwimu kutoka katika Wizara za Kisekta 12, Taasisi tatu (3), Mamlaka za Serikali za Mitaa nane (8) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali matano (5). Kupitia vikao hivyo, Mpango kazi wa mwaka wa utekelezaji kwa kila Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa umeandaliwa na utekelezaji wake unaendelea.

149. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishiriki mkutano wa sita (6) kuhusu Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama uliofanyika

mwezi Desemba, 2025 nchini Tunisia. Mkutano huo uliandaliwa na Uongozi wa Umoja wa Afrika kupitia Ofisi ya Mjumbe Maalum wa Umoja wa Afrika anayeshughulikia masuala ya Wanawake, Amani na Usalama kwa kushirikiana na Serikali ya Tunisia na Mtandao wa Wanawake Viongozi ujulikanao kwa jina la *African Women Leadership Network (AWLN).* Kupitia mkutano huo Tanzania iliahidi kuendelea na utatuzi wa changamoto za wanawake katika nyanja zote na pia kuendelea kuimarisha ushirikiano na umoja wa Afrika na Wadau wengine ili kuhakikisha wanawake wanapata nafasi stahiki katika jitihada zote za ujenzi na ulinzi wa amani.

150. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilizindua Kampeni yenye jina la ***"Inspire to Lead"*** tarehe 07 Julai, 2025 ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kuhamasisha wanawake na wasichana kushiriki na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na maamuzi. Kupitia kampeni hiyo, Wizara imeandaa video fupi 14 za viongozi wanawake wakielezea uwezo wa mwanamke katika nafasi za uongozi kwa ajili ya kutumika kuhamasisha wanawake na wasichana kupitia mitandao ya kijamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-Government Authority - eGA) imeanzisha dirisha maalum katika tovuti ya Wizara liitwalo

**KAMPENI** kwa ajili ya kurusha kampeni zote za Wizara zinazoelimisha jamii. Hadi kufikia mwezi Aprili 2026 kampeni nne (4) zimerushwa kupitia dirisha hilo.

151. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Uratibu wa Wajane, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imehamasisha wajane kuunda vikundi, kuvisajili na kujiunga na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ili waweze kupata fursa za mitaji na masoko. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya vikundi 121 vya wajane vimeanzishwa na kuunganishwa na fursa za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kupata mikopo na taarifa za masoko. Vikundi hivyo vimeanzishwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mtwara, Lindi, Songwe na Dodoma.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imeendelea na ufuatiliaji wa vikundi mbalimbali vya wajane kupitia majukwaa ya Uwezeshaji wanawake kiuchumi na Taasisi zinazotoa huduma kwa wajane kama TAWIA, TUYATA na nyinginezo ili kuhakikisha wajane wanapata haki stahiki na kwa wakati.

153. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishiriki Mkutano wa Wajane Barani Afrika uliofanyika Jijini Windhoek, Namibia mwezi Septemba, 2025. Katika mkutano huo Ujumbe wa Tanzania uliambatana na Mama Anna Mkapa, mjane wa Rais Mstaafu wa awamu ya tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Benjamini William Mkapa. Kupitia Mkutano huo, Mama Anna Mkapa alipata heshima ya kuzindua Mpango wa Afrika wa Ukuaji na Maendeleo ya Wajane (Pan - Africa Widows Growth and Development Initiatives - PAWGADI). Mkutano huo uliazimia kuendeleza jitihada za kutetea, kulinda na kukuza haki na ustawi wa wajane Barani Afrika.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi wenye maono wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanawake wameendelea kujipambanua kama nguzo ya uongozi, umoja wa kitaifa na maendeleo jumuishi. Kwa dhamira hiyo, tarehe 14 Januari, 2026, Wizara ilisajili Women in Leadership Forum (WLF) — Jukwaa la Wanawake Viongozi Tanzania, taasisi ya kipekee iliyoanzishwa na wanawake viongozi 12 kutoka vyama 10 vya siasa, wakiongozwa na muasisi na mbeba maono wake, Mheshimiwa Dkt. Evaline Wilbard Munisi ambaye tupo naye ndani ya Bunge hili,

pamoja na viongozi wenzake ambao wapo katika Jukwaa la Wageni. Ni nadra duniani kuona viongozi kutoka vyama vingi vyenye itikadi tofauti wakivuka mipaka ya ushindani wa kisiasa na kuungana kwa ajili ya amani, mshikamano, uongozi wa wanawake na maslahi mapana ya Taifa. Usajili wa WLF ni kielelezo cha mazingira wezeshi, siasa za staha na falsafa ya Mheshimiwa Rais ya kulileta Taifa pamoja; falsafa inayowafanya wanawake kuwa madaraja ya umoja, sauti za matumaini na wabeba maono ya Tanzania imara na jumuishi.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika ngazi za Mikoa, ambapo Wizara iliungana na Mkoa wa Geita kuadhimisha siku hiyo katika kata ya Kalangalala, Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Geita. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa; ***"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana: Msingi Jumuishi kufikia DIRA 2050***". Kaulimbiu hiyo ilijikita kujenga uelewa wa pamoja ili kuwekeza katika maendeleo jumuishi kwa kutambua na kutekeleza haki za wanawake na wasichana kwa vitendo.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipokea salamu za viongozi na wadau mbalimbali wakiwemo wawakilishi kutoka Benki ya Dunia, Asasi za Kiraia na kwa mara ya kwanza katika

historia ya Tanzania Shirika la Wanawake Viongozi (Women Leaders Forum - WLF) linaloundwa na wanawake waliokuwa wagombea kwa nafasi ya Urais na Makamu wa Rais katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kama nilivyoeleza awali kwenye aya ya 147. Pamoja na ushiriki wao katika maadhimisho hayo pia walihimiza wanawake na wasichana kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni ili kujenga Taifa lenye usawa wa kijinsia lisilokuwa na tofauti za kiitikadi, kidini ama kikabila. Hakika, WLF ni kielelezo cha ukomavu wa demokrasia nchini na alama ya mshikamano wa wanawake pasipo itikadi katika kutafuta maendeleo endelevu.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na maadhimisho hayo, Wizara ilizindua rasmi Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Advancing Gender Equality in Tanzania) unaojulikana kwa jina la "PAMOJA Project". Lengo la mradi huo ni kukuza usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake kiuchumi na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika mikoa 10 yenye jumla ya Halmashauri 40. Maelezo ya kina ya kuhusu Mradi wa PAMOJA yapo katika eneo la kumi linalobainisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli mbalimbali zilifanyika wakati wa maadhimisho katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na kutoa misaada kwenye vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; na kusaidia kaya za watoto wenye ulemavu kwa kutoa misaada ya kifedha na taulo za kike kwa wanafunzi wasichana wa shule za Msingi na Sekondari. Vilevile, kufanya usafi wa mazingira maeneo ya stendi za mabasi; kutoa elimu kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, lishe na malezi bora kupitia mikutano na makongamano; kutoa elimu ya msaada wa kisheria kupitia kampeni ya Mama Samia *Legal Aid Campaign;* na mashindano ya michezo mbalimbali (Bonanza).

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilishiriki kwenye Mkutano wa 70 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Nchini Marekani Mwezi Machi 2026 uliokuwa na kaulimbiu isemayo; ***"Kuhakikisha na Kuimarisha upatikanaji wa haki kwa Wanawake na Wasichana wote, ikiwa ni pamoja na kukuza mifumo ya kisheria yenye usawa na jumuishi, kuondoa sheria, sera na desturi za kibaguzi na kushughulikia vikwazo vya kimuundo".*** Kaulimbiu hiyo imejikita kujadili utekelezaji na jitihada za nchi katika kuimarisha upatikanaji wa haki za

msingi na huduma za kisheria kwa wanawake na wasichana wote.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilifanikiwa kuwasilisha mafanikio yaliyopatikana katika upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana katika mkutano huo. Miongoni mwa wawasilishaji wa Taarifa ya Nchi ni pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria, Chama cha Majaji Wanawake (TAWJA), Shirika la LANDESA na Chama cha Wahandisi Wanawake. Kupitia Mkutano huo nchi ilionesha mafanikio yaliyofikiwa kwa wanawake na wasichana kwa kuakisi utekelezaji wa Mipango na programu za nchi, sambamba na mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** ujumbe wa nchi katika mkutano huo uliambatana na Waziri wa Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar pamoja na viongozi, wataalamu na wanaharakati wanaojihusisha na masuala ya uwezeshaji wanawake, ukatili wa Kijinsia na masuala ya sheria kutoka Wizara za Kisekta, Taasisi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wenye jumla ya washiriki 138. Aidha, Nchi iliandaa mikutano minne (4) ya pembeni, (side events) kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Katiba na Sheria, Chama cha Wanawake Majaji (TAWJA) na Taasisi ya Wahandisi (Kitengo cha Wanawake Wahandisi) ambao walitumia

majukwaa hayo kuelezea utekelezaji wa nchi sanjari na kaulimbiu ya mwaka huu.

162. ***Mheshimiwa spika,*** kupitia Mkutano huo, nchi yetu ilipata mialiko ya kushiriki mikutano mbalimbali kutoka nchi nyingine ikiwa ni pamoja na mkutano ulioandaliwa na nchi ya Misri, Liberia, Morrocco, Uholanzi (Netherland), Uingereza (United Kingdom), Sweeden, Ujerumani, FAO na mikutano iliyoandaliwa na Afrikan Union (AU) na United Nations (UN). Majukwaa hayo yalisaidia kutambua fursa na namna ya kutatua changamoto zinazohusu masuala ya uimarishaji na upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuleta ufanisi na uendelevu wenye tija wa mikutano hii, Wizara imeratibu kikao cha tathimini na Wadau wote walioshiriki mkutano huo tarehe 09 Mei, 2026 ambapo wadau walijadili mafanikio, changamoto na mikakati ambayo itazingatiwa katika mikutano ijayo hususan mkutano wa 71 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani. Aidha, katika mkutano huo ulizinduliwa Mwongozo wa Kuratibu Ushiriki wa Wadau wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa wa mwaka 2024 ambao utasaidia kuratibu ushiriki wa

mikutano hiyo kabla, wakati na baada ya kufanyika kwa mikutano hiyo kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa maendeleo.

**ENEO LA 7: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

164. ***Mheshimiwa Spika,*** usajili na uratibu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni majukumu muhimu yanayotekelezwa na Wizara, ili kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya kikatiba ya kujumuika na kuchangia maendeleo kwa kutoa huduma kwa jamii zenye uhitaji. Uratibu wa Mashirika haya umeendelea kuimarisha mahusiano kati Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika utekelezaji wa miradi na utambuzi wa mchango wa Mashirika hayo katika maendeleo ya nchi. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini yanasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 na Kanuni zake.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,066 (Kimataifa 49, Kitaifa 973, Kimkoa 23 na Kiwilaya 21) yamesajiliwa kati ya Mashirika 1,000 yaliyopangwa kusajiliwa. Mafanikio hayo yamechangiwa na uboreshaji wa huduma za

usajili kupitia mfumo wa kielektroniki na kutanua wigo wa watumiaji wa mfumo huo. Mashirika yaliyosajiliwa yamejikita katika utekelezaji wa afua za sekta mbalimbali za maendeleo ikiwemo uwezeshaji wa jamii kiuchumi, afya, mazingira, elimu, ulinzi wa jamii, kilimo, utawala bora, maji, miundombinu, haki za binadamu na jinsia.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wasajili Wasaidizi waliopo ngazi za Halmashauri na Mikoa imeendelea kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo katika kipindi husika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,547 yalifikiwa katika Halmashauri 154 nchini. Ufuatiliaji huo ulibainisha kuwa kati ya Mashirika yaliyofuatiliwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,432 yanatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayosimamia uendeshaji wa Mashirika hayo, pamoja na vipaumbele vya Taifa. Aidha, Mashirika 115 yalibainika kutozingatia Sheria na taratibu za uendeshaji wake kwa kutowasilisha taarifa za mwaka. Mashirika hayo yamejengewa uwezo na kupewa muda maalum wa kuwasilisha taarifa hizo ili kuendana na matakwa ya Sheria.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inashirikiana na Wizara ya Fedha katika uratibu wa pamoja na ufuatiliaji wa miradi yenye uendelevu ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kwa mujibu wa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara (2025). Kupitia ufuatiliaji huo, mwaka 2025/2026 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 250 yalifuatiliwa katika mikoa 10 ya Kilimanjaro, Mbeya, Dodoma, Arusha, Iringa, Manyara, Tanga, Mwanza, Tabora na Dar es Salaam. Ufuatiliaji huo ulilenga kuhakiki utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye uendelevu na kutathmini tija ya miradi hiyo kwa jamii.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ufuatiliaji huo, ilibainika kuwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalipokea jumla ya shilingi bilioni 296.5. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 275.6 sawa na asilimia 93 zilitoka katika vyanzo vya nje ya nchi na shilingi bilioni 20.9 sawa na asilimia 7 zilitoka katika vyanzo vya ndani ya nchi. Aidha, tathmini hiyo ilionesha kuwa Mashirika mengi yanajiendesha kwa kiasi kikubwa kwa kutegemea ufadhili kutoka nje ya nchi ambapo kwa sasa wafadhili wengi wamepunguza ufadhili.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutegemea wafadhili, baadhi ya Mashirika

yameendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 - 2026/27). Mkakati huo unahimiza Mashirika kuwekeza mitaji katika miradi ya kijamii yenye kujiendesha kibiashara ili kuongeza uendelevu wa shughuli zao. Kwa mfano, Shirika la *Ilula Orphan Program (IOP)* la Mkoani Iringa limekuwa la mfano katika utekelezaji wa Mkakati huo ambapo kati ya shilingi bilioni 3 inazotumia katika uendeshaji wa shughuli zake, bilioni 1.8 sawa na asilimia 60 zinatokana na miradi ya uendelevu ya Shirika ambayo ni shule, chuo cha ufundi, nyumba za malazi pamoja na miradi ya kilimo na ufugaji. Miradi hiyo imechangia utoaji wa huduma kwa jamii na kutoa ajira kwa wananchi wa maeneo hayo.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kupitia **Mradi wa Wajibika** unaofadhiliwa na Ubalozi wa Uswisi na Ubalozi wa Uingereza imeandaa mwongozo wa utekelezaji wa Mkakati huo. Mwongozo huo unalenga kuongeza uelewa kuhusu uhimilivu na uendelevu wa Mashirika hayo pamoja na kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mkakati huo. Kutokana na juhudi hizo baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameanzisha Taasisi za Fedha zinazotoa mikopo hususani kwa wanawake na vijana.

Mashirika hayo ni Shirika la *World Vision* Tanzania iliyoanzisha *VisionFund* Tanzania, Shirika la BRAC Maendeleo lililoanzisha BRAC Tanzania *Finance Limited* na Shirika la Pastoral Women's Council (PWC) lililoanzisha *Engison Microfinance Limited*.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali za kupunguza utegemezi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa wafadhili wa nje na kuimarisha uendelevu wa Mashirika hayo, Serikali imezindua Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Mchakato wa Uanzishwaji wa Mfuko wa Pamoja wa Ruzuku kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs Basket Fund - NBF). Kamati hiyo inaongozwa na Dkt. Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB. Mfuko huo utayawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupata rasilimali fedha zitakazoratibiwa kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi visivyo na masharti magumu. Kamati hiyo inatarajia kukamilisha kazi hiyo ndani ya mwaka ujao wa fedha 2026/27.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2025 ikitoa taarifa ya mchango wa Mashirika hayo kwa mwaka 2024 kwa mujibu wa utaratibu wa utoaji wa taarifa hizo. Taarifa hiyo ilionesha kuwa, jumla ya

shilingi trilioni 1.2 zilitumika katika shughuli za utekelezaji wa miradi. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 980.3 kilitumika kutekeleza miradi ya afya, nishati, mazingira, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, elimu, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu na jinsia na kiasi cha shilingi bilioni 219.7 kilitumika kwa ajili ya shughuli za kiutawala za Mashirika hayo. Aidha, tathimini hiyo ilibaini kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametoa ajira 18,529 ambapo wanawake walikuwa 10,504 na wanaume 8,025. Vilevile, afua zilizotekelezwa na Mashirika hayo zimenufaisha wananchi 208,300.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** Waratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ngazi za Mikoa na Hamashauri ni Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi hizo ambao ndio Wasajili Wasaidizi. Katika kuhakikisha kada hiyo inajengewa uwezo kuhusu uratibu wa Mashirika hayo, Wizara imewajengea uwezo Wasajili Wasaidizi 210 wa Mikoa na Halmashauri zote nchini. Aidha, Wajumbe 30 wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), pamoja na Wawakilishi 2,636 wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pia wamejengewa uwezo kuhusu Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara (2025), Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti

ya Serikali (2025/26), Mwongozo wa Uzingatiaji wa Uwazi wa Masuala ya Kifedha na Ushirikiano kati ya Serikali na Asasi Zisizo za Serikali (2025), pamoja na Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha kuandaa miradi yao kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa na kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwenye Bajeti ya Serikali.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026**,** Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) iliratibu Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Jijini Dodoma. Kupitia jukwaa hilo huduma mbalimbali zilitolewa kwa wananchi ikiwemo huduma ya msaada wa Kisheria ambapo wananchi 2,094 walifikiwa na kwamba migogoro ya ardhi 50 ilishughulikiwa. Aidha, wananchi 138 (Wanaume 77 na Wanawake 61) walipata huduma ya afya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kurudisha kwa jamii

175. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana kwa karibu na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini katika kuimarisha uratibu wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kujenga

ushirikiano madhubuti, kuongeza uwajibikaji na kuimarisha mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa. Katika kuendeleza juhudi hizo, tarehe 22 Aprili, 2026, Wizara iliratibu kikao maalum cha Wabunge wa Viti Maalum wanaowakilisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ajili ya kupitia taarifa ya utekelezaji pamoja na mwelekeo wa Sekta hiyo. Kikao hicho kilitoa fursa muhimu ya kujadili mafanikio yaliyopatikana, changamoto zinazoikabili Sekta, pamoja na mikakati ya kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na kuchochea maendeleo jumuishi ya Taifa. Aidha, kikao hicho kilisisitiza umuhimu wa kuongeza utambuzi wa mchango unaotolewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya jamii, ustawi wa wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

176. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia majadiliano hayo, mrejesho ulionesha kuwa, kati ya hoja 19 zilizowasilishwa na Sekta kupitia majukwaa mbalimbali ya mwaka, hoja 15 sawa na asilimia 80 tayari zimefanyiwa kazi na Serikali. Mafanikio hayo yanajumuisha kuimarishwa kwa utendaji wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) pamoja na kuboreshwa kwa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini ili

kuyawezesha Mashirika hayo kushiriki kikamilifu katika vikao rasmi vya Serikali katika ngazi za Halmashauri, Wilaya na Mikoa. Hatua hizi zinaendelea kuimarisha mazingira wezeshi ya ushiriki wa wadau katika maendeleo na kuifanya Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa mshirika muhimu wa Serikali katika kufanikisha agenda ya maendeleo ya Taifa kuelekea DIRA 2050.

177. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na mafanikio hayo, Wizara inapenda kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan**, kwa uamuzi wake wa kizalendo, wenye maono na tija kwa Taifa wa kuongeza idadi ya Wabunge wanaowakilisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka wawili hadi watatu. Uamuzi huo ni hatua kubwa na ya kihistoria inayoonesha dhamira thabiti ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuendelea kuimarisha ushiriki wa wadau wa maendeleo katika ujenzi wa Taifa, kuongeza uwakilishi wa sauti za wananchi na kuipa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nafasi pana zaidi ya kushiriki katika majadiliano na maamuzi muhimu ya kitaifa. Hatua hiyo imekuwa ni chachu muhimu ya kuimarisha mahusiano kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuongeza ari ya

uwajibikaji wa Sekta hiyo, na kuifanya kuwa mshirika imara zaidi katika utekelezaji wa agenda ya maendeleo ya Taifa kuelekea DIRA 2050.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa ushirikiano kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mamlaka za Serikali katika ngazi za Mikoa kumewezesha kufungamanisha agenda za maendeleo za Mashirika hayo na vipaumbele vya maendeleo vya Mikoa husika, hali inayoongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi na mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya Taifa. Sambamba na mafanikio hayo, Wizara inaendelea kushirikiana kwa karibu na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kushughulikia hoja zilizobakia ikiwemo kuharakisha upatikanaji wa vibali vya utekelezaji wa miradi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuhakikisha maombi ya msamaha wa kodi yanawasilishwa na kupatiwa mrejesho kwa wakati kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania, hatua ambazo zinalenga kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji wa Mashirika hayo na kuyawezesha kuchangia kwa ufanisi zaidi katika kufanikisha DIRA ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayohitaji mshikamano wa dhati wa wadau wote wa maendeleo wakiwemo Asasi za Kiraia.

## ENEO LA 8: URATIBU WA MPANGO KAZI WA TAIFA WA KUTOKOMEZA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO AWAMU YA PILI (MTAKUWWA II)

179. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya Pili (MTAKUWWA II – 2024/25 - 2028/29) wenye lengo la kuhakikisha jamii inakuwa huru dhidi ya vitendo wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto na inapata fursa sawa za kushiriki katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mpango huu una maeneo makuu nane (8) ambayo ni (i) Kuimarisha Uchumi wa Kaya; (ii) Mila na Desturi; (iii) Mazingira Salama katika Maeneo ya Umma na Mtandaoni; (iv) Malezi, Familia na Mahusiano; (v) Usimamizi na Utekelezaji wa Sheria; (vi) Utoaji wa Huduma za Mwitikio kwa Wahanga wa Ukatili; (vii) Ulinzi wa Mtoto Shuleni na Stadi za Maisha; na (viii) Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Washirika wa Maendeleo imeendelea kuratibu utekelezaji wa mpango huo ili kuimarisha utekelezaji wa afua mbalimbali. Mpango huo ni shirikishi kwa

kuhusisha Serikali, Washirika wa Maendeleo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi Binafsi na jamii kwa ujumla. Aidha, Mpango huo unasisitizwa kujadiliwa katika ngazi za maamuzi ikiwemo Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC), Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) na Kamati za Ushauri za Mikoa (RCC) zinazoongozwa na Wakuu wa Mikoa na zinazoongozwa na Wakuu wa Wilaya.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango huo kwa kila eneo unaratibiwa na Wizara mbalimbali kulingana na usimamizi wa Kisera wa eneo husika ambapo, eneo la kuimarisha uchumi wa kaya linaratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuwezesha mazingira ya upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa makundi ambayo yapo katika sekta isiyo rasmi hususan wananchi wasio na sifa za kuweza kupata mikopo mikubwa katika Taasisi za Fedha.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** fursa hizo ni pamoja na mikopo isiyo na riba kutokana na mgawanyo wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri, Mikopo ya wafanyabiashara ndogondogo, ushiriki wa Makundi maalum katika zabuni za manunuzi ya Umma, ushiriki wa wanawake katika Majukwaa ya Uwezeshaji

Wanawake Kiuchumi na uwepo wa madirisha ya mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake yaliyopo katika Benki mbalimbali hapa nchini. Vilevile, eneo hili linatambua pia Mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania - TASAF ambapo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, mfuko umetoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 43.5 kwa Kaya zilizotambuliwa 896,746 katika maeneo 186 ya utekelezaji wa programu ya TASAF.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mpango huo Wizara inaratibu pia eneo la kuimarisha Mila na Desturi kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ambayo imezindua. Miongoni mwa kazi zinazofanyika katika eneo hili ni pamoja na kuendesha majadiliano ya mmomonyoko wa maaadili ngazi ya jamii kuhusu mila na desturi kwa lengo la kushawishi jamii kubadili mitazamo na kuachana na mila na desturi hasi zinazochochea ukatili wa kijinsia.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** majadiliano hayo yamefanyika katika Mikoa 10 ambayo ni Manyara, Mara, Shinyanga, Geita, Arusha, Singida, Mwanza, Simiyu, Lindi na Tanga ambapo jumla ya washiriki 19,215 (Wanaume 10,560 na Wanawake 8,655) wa rika na nyadhifa mbalimbali walifikiwa. Makundi yaliyofikiwa ni

wazee wa mila (350), Ngariba (15), Viongozi wa dini (200), watu mashuhuri (50), Viongozi wa Kisiasa (100), Watumishi wa Serikali (500), na Wananchi wa kawaida (18,000). Kupitia majadiliano hayo, jamii zilitambua baadhi ya mila zenye madhara na kuweka mikakati mbalimbali ya kuzitokomeza. Aidha, katika kuimarisha masuala ya maadili pia, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo imezindua **Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmmonyoko wa Maadili (2026/27 – 2036/37)** unaolenga kujenga jamii yenye maadili, uzalendo, uwajibikaji, na mshikamano wa kitaifa.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Mipango hii miwili (2) yaani Mpango wa MTAKUWWA na Mkakati wa Kupambana na Mmomonyoko wa Maadili ni Mipango pacha ambayo inalenga kuhakikisha jamii ya Tanzania inakuwa salama dhidi ya ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya watoto pamoja na kuimarisha mila, desturi na tamaduni chanya miongoni mwa jamii.

***Nitoe pongezi zangu za Dhati kwa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo inayoongozwa na Mhe. Paul Makonda (Mb.) kwa kuona umuhimu wa kupambana na mmomonyoko wa maadili na kuandaa Mkakati huo.***

186. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, imewajengea uwezo wataalam mbalimbali kuhusu mbinu za kuelemisha jamii katika masuala mbalimbali ikiwemo: Fursa za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kutokomeza Mila na Desturi zenye Madhara; Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Sheria; Kuanzisha Dawati la ulinzi wa Mtoto Shuleni; na kuanzisha Dawati la Jinsia katika Maeneo ya Umma. Mafunzo haya yalitolewa kwa jumla ya Wataalamu 238 kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Wataalamu waliojengewa uwezo ni Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa TEHAMA, Watangazaji wa Redio za Kijamii, Maafisa Habari wa Serikali, Viongozi wa Kidini na Viongozi wa Kimila. Kupitia mafunzo hayo, masuala mbalimbali yaliibuliwa na kujadiliwa na wataalamu hao ikiwemo namna ya kukabiliana na mila zenye madhara.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafunzo hayo, jumbe mbalimbali ziliandaliwa kwa lengo la kuelimisha jamii ikiwemo ujumbe usemao ***"Tuseme Hapana kwa Ukatili wa Kijinsia, mila na desturi zinazozuia heshima na ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika maendeleo ya familia na Taifa. Usawa kwa Wote Maendeleo kwa Taifa"***. Aidha, waandishi na watangazaji wa

redio mbalimbali za kijamii walishiriki mafunzo hayo na wameanza kurusha maudhui ya kuelimisha jamii kulingana na maeneo waliojengewa uwezo. Wanahabari hao walitoka katika vituo vya redio za Mpanda FM (Katavi), Joy Radio (Kigoma), Nyemo FM (Dodoma), CG FM (Tabora), Afya Radio (Mwanza), Kasibante FM Radio (Kagera), Mazingira FM (Mara), Sunrise Radio (Arusha), Mbeya Highlands FM (Mbeya), Nuru FM (Iringa), Abood FM (Morogoro), Hopaje FM (Mtwara) na Ruangwa FM (Lindi).

***Nitoe Rai kwa Waandishi wa Habari katika Maeneo yote ikiwemo Waandishi wa Habari wa Mtandaoni kutumia Taaluma zao kutangaza Habari zenye kuelimisha na kuhabarisha ili kujenga jamii yenye uelewa mpana na si kutangaza na kurusha maudhui yanayochangia mmomonyoko wa maadili kwa lengo la kupata wafuasi wengi katika vyombo vyao na kusababisha mmomonyoko wa maadili.***

188. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu kikao ngazi ya Mawaziri kwa lengo la kujadili hali ya maadili katika jamii kufuatia ongezeko la matukio ya ukiukwaji wa maadili katika jamii. Aidha, kikao hicho pia kilijadili athari za matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, changamoto zinazokwamisha juhudi za kudhibiti mmomonyoko wa maadili, pamoja na kuweka

maazimio kuhusu hatua stahiki kudhibiti hali hiyo.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** kikao hicho kilihudhuriwa na Mawaziri kutoka Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Afya; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Fedha; Wakuu wa Taasisi kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); pamoja na Wakurugenzi na wataalam kutoka Wizara hizo.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kikao hicho, masuala mbalimbali yanayochochea mmomonyoko wa maadili yalijadiliwa ikiwemo: -

i) Kufanya mapitio ya Sera na Sheria zote zinazoendana na masuala ya maadili kwa lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti na kuanisha adhabu kwa makosa yanayochochea mmonyoko wa maadili;

ii) Kuimarisha utekelezaji wa sheria kwa kuwachukulia hatua watuhumiwa wote watakaobainika kuvunja sheria au kuchochea mmomonyoko wa maadili kwa namna yoyote ile;

iii) Kuongeza ushirikiano wa Wizara na Taasisi zote zenye mamlaka ya kudhibiti mmomonyoko wa maadili ikiwemo Mamlaka ya Mawasiliao Tanzaia TCRA na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA);

iv) Kuhakikisha masuala ya mmomonyoko wa maadili yanajadiliwa katika vikao mbalimbali vya maamuzi kuanzia ngazi ya Taifa, hadi Kamati za Ushauri za Mikoa (RCC), Wilaya (DCC) na ngazi Kata (WDC); na

v) Kuandaliwa kwa Mpango Kazi jumuishi wa utekelezaji wa afua za kupambana na mmomonyoko wa maadili.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuanza utekelezaji wa hatua za haraka za kupambana na mmomonyoko wa maadili, Serikali imefanya utambuzi wa baadhi ya matukio yanayochochea mmomonyoko wa maadili ambapo orodha ya watuhumiwa wanaohusika kwenye matukio hayo imeandaliwa na kuwasilishwa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya hatua zaidi.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, katika kuimarisha jitihada za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili; Serikali imeandaa **Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania (2022)** na **Mwongozo wa**

**Uzingatiaji Maadili katika Kazi za Sanaa (2023)**. Miongozo hiyo ni jitihada za pamoja katika kuimarisha maadili na misingi ya utamaduni wa Taifa na kudhibiti maudhui ya kazi za sanaa zinazochochea mmomonyoko wa maadili yasiyoendana na mila na desturi za Kitanzania.

***Nitoe rai, kwa jamii kwamba suala la maadili sio ajenda ya Serikali peke ya yake bali ni ajenda ya Taifa kwa ujumla, hivyo ni wajibu wetu sote kulinda maadili ya Taifa letu kwani Taifa ni letu na maadili ni ya kwetu kama ilivyoainishwa katika misingi ya DIRA 2050 kuwa na Taifa linalohifadhi, kukuza na kulinda maadili na tamaduni chanya kwa lengo la kuimarisha umoja na utambulisho wa kitaifa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo***.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Mazingira Salama Katika Maeneo ya Umma na Mtandaoni ni eneo lingine la MTAKUWWA II ambalo linalenga kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii. Mazingira hayo yanajumuisha maeneo ya kijiografia yanayokutanisha watu wengi kupata huduma kama vile sokoni, vituo vya usafiri, viwanja vya michezo na fukwe pamoja na maeneo ya mtandaoni. Eneo hili linaratibiwa na OWM – TAMISEMI pamoja na Wizara ya

Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha usalama katika mazingira hayo ikiwemo, ujenzi wa mfumo wa kutambua matukio na kuhifadhi takwimu za Uhalifu Mtandaoni na kuimarisha mazingira ya TEHAMA katika maabara za Jeshi la Polisi Tanzania na Kitengo cha Uchunguzi wa Kidijitali (Cybercrime Unit). Hatua hizi zinalenga kuongeza uwezo wa uchunguzi wa uhalifu mtandaoni na kuimarisha usalama wa matumizi ya mifumo ya kidijitali hususan kukabiliana na ukatili wa mtandaoni.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo lingine la Huduma na Msaada wa Kisheria linaloratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria, Mpango umetambua jitihada za Serikali na wadau wengine ikiwemo utoaji huduma ya Msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Mama Samia *Legal Aid Campaign*. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya wananchi 7,462,387 (Wanaume 3,611,286 na Wanawake 3,851,101) walifikiwa na kupatiwa huduma za msaada wa kisheria.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa manusura wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, Wizara inaratibu kituo cha Kijamii cha Huduma kwa Wateja (Community Contact

Center) chenye lengo la kusogeza huduma kwa jamii. Kupitia kituo hicho, wananchi wanaweza kupiga simu bure kwa ajili ya kupata huduma zinazoratibiwa na Wizara au kutoa taarifa ya changamoto mbalimbali. Namba za kituo cha Wizara ni **0262160250, 0734986503, 0766400168, 0769608130, 0774112233**.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya mashauri 753 yalipokelewa kupitia kituo cha kijamii cha huduma kwa wateja. Kati ya mashauri yaliyopokelewa, mashauri 660 yamefanywa kazi na kufungwa na mashauri 93 yanaendelea kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya mashauri yaliyopokelewa, mashauri 272 yalihusu huduma za ustawi wa jamii ikiwemo masuala ya ndoa na familia, ukatili wa kijinsia, mahitaji ya msaada wa afya ya akili na kisaikolojia, malezi ya kambo na kuasili pamoja na usajili wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana; Mashauri 101 yalihusu masuala mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo ambapo; Mashauri 373 yalihusu Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Mashauri mawili (2) yalihusu masuala ya kijamiii; na Mashauri Matano (5) yalihusu huduma za maendeleo ya mtoto.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo la Ulinzi wa Mtoto Shuleni na Stadi za Maisha linaratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo mambo mengi yamefanyika katika kuimarisha ulinzi wa mtoto shuleni. Miongoni mwa masuala yaliyofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu 6,024 wa shule za awali na shule za msingi kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia kupitia mpango wa shule salama kwa lengo la kuboresha huduma za malezi, ushauri na unasihi shuleni. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha masuala mtambuka ikiwemo mazingira, usawa wa kijinsia na elimu ya afya katika taasisi za elimu ya juu kwa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 34,000 kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili na kupinga ukatili wa kijinsia ili kufanya vyuo kuwa sehemu salama ya kuishi, kufanya kazi na kupata ujuzi na mafunzo.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo la Uratibu wa MTAKUWWA linafanyika kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Katika kuimarisha uratibu wa MTAKUWWA, Wizara imeandaa Mwongozo wa uratibu wa MTAKUWWA II (2024/25 -2028/29) unaofafanua kwa kina majukumu ya utekelezaji wa mpango kwa

ngazi zote. Malengo ya mwongozo huo ni pamoja na kuimarisha uratibu wa mpango; kuimarisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto; na kuimarisha utoaji wa huduma za msaada kwa wahanga na waathirika vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeandaa Kitini cha Mafunzo (Training Manual) na Kitabu cha Mshiriki kwa ajili ya Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika ngazi zote. Lengo ni kuimarisha uelewa na uwezo wa wajumbe wa kamati hizo katika kutekeleza majukumu yao. Nyenzo hizo zipo katika hatua ya majaribio kabla ya kuanza kutumika.

201. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI imeratibu uandaaji wa Mipango Mikakati ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele maalum vya kila mkoa. Hadi kufikia Aprili, 2026 Mikoa 10 ya Mwanza, Geita, Dodoma, Iringa, Mbeya, Njombe, Shinyanga, Songwe, Dar es Salaam na Mtwara imeandaa na kuzindua mipango hiyo, na mikoa 16 ipo katika hatua za ukamilishaji. Mipango ya MTAKUWWA ngazi ya Mkoa inaimarisha utekelezaji wa kukabiliana na

kupunguza vitendo vya ukatili kwa kuzingatia mahitaji na mazingira ya Mkoa husika.

202. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utekelezaji wa MTAKUWWA, jumla ya vikundi kazi nane (8) vimeundwa kwa kuzingatia maeneo ya utekelezaji wa mpango. Ili kuongeza ufanisi wa vikundi kazi hivyo, Wizara imeandaa hadidu za rejea (Terms of Reference – TOR) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa wajumbe wanaounda vikundi kazi hivyo. Vilevile, Wizara imefanya uzinduzi wa Vikundi Kazi hivyo kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa afua za mpango, pamoja na kuimarisha uratibu, ushirikiano na mawasiliano kati ya waratibu wa vikundi kazi na wadau mbalimbali. Uzinduzi wa vikundi kazi ulifanyika mwezi Februari, 2026 ambapo Wakuu wa Vikundi kazi walipata fursa ya kueleza utekelezaji, mafanikio changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha utekelezaji wa mpango.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI imewajengea uwezo Wakuu wa Idara za Mipango na Uratibu 184 kutoka Halmashauri zote nchini kuhusiana na umuhimu wa kutenga fedha za utekelezaji wa MTAKUWWA katika maeneo yao. Mafunzo hayo ni miongoni mwa utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti

ya Serikali wa mwaka 2026/27 unaoelekeza Maafisa Masuhuli kutenga fedha za utekelezaji wa MTAKUWWA.

***Nitoe Rai wa Waheshimiwa Wabunge kufuatilia utekelezaji wa ajenda ya MTAKUWWA katika vikao rasmi ambavyo Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe wa kudumu ikiwemo vikao vya ushauri ngazi ya Mikoa na Wilaya ili kuhimiza utengaji wa Bajeti na kufuatilia utekelezaji wa MTAKUWWA katika Majimbo yao.***

## ENEO LA 9: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA.

204. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbili (2) zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Maelezo ya kina kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo: -

### *TAASISI YA USTAWI WA JAMII*

205. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Ustawi wa Jamii ya Taifa Na. 26 ya mwaka 1973, kwa lengo la kuandaa

rasilimali watu wenye sifa stahiki kwa ajili ya kuimarisha muundo wa utoaji wa huduma za kijamii nchini. Taasisi imepitia maboresho na mabadiliko mengi ambapo kwa sasa Taasisi inatoa huduma mbalimbali za ustawi wa jamii zikiwemo: mafunzo ya kada ya ustawi wa jamii kuanzia ngazi ya cheti hadi uzamili; tafiti za kijamii; na kutoa utaalamu elekezi unaohusiana na masuala ya ustawi wa jamii. Taasisi hii ina kampasi mbili (2) ambapo kampasi kuu ipo eneo Kijitonyama, Jijini Dar es Salaam na Kampasi nyingine ipo eneo la Kisangara, Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii ina programu 20 za mafunzo, ambapo katika mwaka wa masomo 2025/26, hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 imesajili jumla wanafunzi 5,868 (Wanaume 2,045 na Wanawake 3,823) ikilinganishwa na wanafunzi 5,400 (Wanaume 1,871 na Wanawake 3,529) walisajiliwa katika mwaka wa masomo 2024/2025. Wanafunzi wapya waliodahiliwa kati ya hao ni 3,000 (Wanaume 1,028 na Wanawake 1,972). Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na wanafunzi 2,731 (Wanaume 1,022 na Wanawake 1,709) waliodahiliwa mwaka wa masomo 2024/25.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imefanikiwa kuhuisha mitaala ya kozi ya Ustawi wa Jamii kwa Ngazi ya Cheti na Diploma (NTA 4, 5 na 6). Mitaala hiyo tayari imethibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) na imeanza kutumika Novemba, 2025 ambapo inatarajiwa kufikia ukomo wa matumizi ifikapo Desemba, 2030.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 jumla ya wanafunzi 3,121 (Wanaume 1,108 na Wanawake 2,013) wamehitimu masomo yao ikilinganishwa na wanafunzi 3,112 (Wanaume 1,028 na Wanawake 2,084) waliohitimu katika mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 0.3.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ina Kituo kinachotoa Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia. Katika kipindi husika jumla ya wananchi 403 (Wanaume 190, Wanawake 213) ambapo kati ya hao wananchi 356 (Wanaume 169, Wanawake 187) na watumishi 47 (Wanaume 31 na Wanawake 16) wa Taasisi mbalimbali za Serikali walipata elimu, ushauri na msaada wa kisaikolojia.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inaratibu programu ya uanagenzi yenye lengo la kuwasaidia wahitimu kupata ujuzi wa vitendo na uzoefu unaohitajika katika fani walizohitimu. Katika

kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya wahitimu 21 walishiriki programu hiyo kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo Manispaa ya Tabora, Halmashauri ya Jiji la Ilala, Kituo cha Utetezi wa Haki za Binadamu pamoja na Shirika la *Plan International.* Aidha, hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya wanafunzi 35 walipata ajira kupitia fursa inayotolewa na Programu hiyo.

***TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU***

211. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ilianzishwa mwaka 1963 kama Kituo cha kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabwana na mabibi maendeleo waliokuwa na jukumu la kuhamasisha maendeleo ngazi ya jamii. Taasisi hii imepitia maboresho na mabadiliko mengi ambapo kwa sasa inajishughulisha na masuala mengi ya kijamii ikiwemo utoaji wa mafunzo ya kada ya Maendeleo ya Jamii kuanzia ngazi ya Cheti hadi Uzamili; kufanya utafiti mbalimbali wa masuala ya kijamii; na kutoa ushauri elekezi.

212. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ina programu 50 za mafunzo, ambapo hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya wanafunzi 3,648 (Wanaume 1,469 na Wanawake 2,179) walidahiliwa. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12 ikilinganishwa na

udahili wa mwaka wa masomo 2024/25, ambapo wanafunzi 3,219 (wanaume 1,286 wanawake1,933) walidahiliwa.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26 Taasisi ilifanya mahafali ya 15 ambapo jumla ya wanafunzi 1,813 (Wanaume 758 na Wanawake 1,055) walihitimu. Idadi hii ya wahitimu imeongezeka kwa asilimia 9.8 ikilinganishwa na wahitimu wa mwaka 2024/25, ambapo wanafunzi 1,672 (Wanaume 554 na Wanawake 1,118) walihitimu.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidigitali (Jamii Outreach Digital Innovation Center – JODIC), Taasisi imetekeleza dhana tatu (3) ambazo ni Uanagenzi, Ushirikishwaji Jamii na Ubunifu. Jumla ya wanafunzi 2,445 walipata mafunzo na kuunganishwa na mashirika kwa ajili ya kuongeza ujuzi kulingana na taaluma zao ili iwasaidie kujiajiri, kuajiriwa na kuajiri wengine.

215. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu dhana ya ushirikishwaji jamii, wanafunzi wa Taasisi hushiriki na jamii inayowazunguka katika kubaini changamoto zinazoikabili na kuzitafutia utatuzi ambapo katika kipindi hiki elimu ya upimaji wa VVU/UKIMWI ilitolewa kwa watu

420 katika kijiji cha Patandi ambapo watu 66 walipima kwa hiari.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kuhusu dhana ya ubunifu, wanafunzi watatu (3) waliwezeshwa kushiriki mashindano ya *Afrinnovate Youth Challenge Competition* yaliyoandaliwa na Taasisi ya *E3 Empowered Africa* yaliyoshirikisha vyuo vikuu na vyuo vya kati kumi kutoka Tanzania. Mashindano hayo yalilenga kuibua bunifu zinazosaidia wanafunzi kuweza kujiajiri, kuajiriwa na kuajiri wengine ambapo bunifu zao zilihusisha teknolojia ya kubangua karanga. Wanafunzi wa Taasisi waliibuka washindi wa kwanza na kupata zawadi ya Dola za Kimarekani 3,500. Aidha, wanafunzi hao walishinda pia mashindano ya *Afrinnovate Youth Challenge Competition* ya Afrika na kuwa washindi wa kwanza barani Afrika na kuzawadiwa Dola za Kimarekani 5,000.

217. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kituo cha Kitaifa cha utafiti na uhifadhi wa machapisho ya wanawake (National Women's Research and Documentation Center - NWRDC) imefanyika midahalo 10 kuhusu fursa za ubunifu na ujasiriamali katika Taasisi nane (8) za elimu ambapo jumla ya wanafunzi 969 (Wanaume 487 na Wanawake 482) walifikiwa na hivyo kuongeza uelewa, kujiamini na kutambua

fursa zinazowazunguka ili kukabiliana na changamoto zilizopo.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kilifanya tafiti mbili (2) zinazohusu ukatili wa kijinsia na kimewezesha utoaji wa msaada wa kisheria kwa wanawake 15 katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, ambapo wanawake wenye kipato kidogo na wasiokuwa na fursa ya kuwalipa mawakili walipewa ushauri wa kisheria na taratibu za kufuata ili kupata haki zao. Vilevile, mafunzo ya uongozi yametolewa kwa wanafunzi wa kike 40 katika vyuo vikuu na vyuo vya kati sita (6), ambapo mafunzo hayo yamesaidia wanafunzi kuongeza uelewa wa misingi ya uongozi bora, kujiamini, ubunifu na kuwaandaa kuwa viongozi wa baadae wenye weledi na kujituma.

## ENEO LA 10: UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

219. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo nane (8) ikijumuisha miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Taasisi, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vituo vya Ustawi wa Jamii; na miradi ya kutoa huduma katika jamii.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama, ambapo mradi huo umefikia asilimia 85 ya utekelezaji. Mradi huu unakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi 626,405,367.66, ambapo hadi sasa shilingi 366,119,211.65 zimeshatumika. Hatua hii inaendelea kuimarisha ubora wa miundombinu na mazingira ya kitaaluma ndani ya Taasisi.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya utendaji kwa watumishi, Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru lenye Ofisi 44 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 94 na kumbi tano (5) zenye uwezo wa kuhudumia watu 545. Jengo hilo litagharimu shilingi bilioni 5.7, ambapo katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imepokea shilingi bilioni 1.2, na kufanya jumla ya shilingi bilioni 3.9 zimetolewa katika mradi husika na kufanya utekelezaji wa mradi huo kufikia asilimia 71.

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na ujenzi wa hosteli ya Wasichana ya ghorofa mbili (2) yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 600 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole, ambapo hadi kukamilika Mradi huu

utagharimu kiasi cha shilingi Bilioni 5.1. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/26 Mradi huu umepokea shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa awamu ya tatu (3) na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa tangu mradi huo kuanza Mwezi Aprili, 2022 kuwa ni shilingi bilioni 2.6. Aidha, utekelezaji wa mradi huo umefika asilimia 65 ya ujenzi.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza mradi wa Ujenzi wa Hosteli Katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli unaokadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.7 hadi kukamilika ikijumuisha na gharama za ununuzi wa samani. Hosteli hiyo ya wasichana ya ghorofa tatu (3) itakuwa na uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 576. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/26 kiasi cha shilingi milioni 600 kimepokelewa na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa katika mradi huo kuwa ni shilingi Bilioni 2.1 ambapo utekelezaji wa mradi huo umefika asilimia 67 ya ujenzi.

224. ***Mheshimwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Upangaji wa Rasilimali za Kutekeleza Afua za Kijinsia (Resource Planning for Gender Project). Mradi huu unalenga kutekeleza shughuli za kutokomeza ukatili wa kijinsia pamoja na kuwezesha uratibu wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya

Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II 2024/25 – 2028/29).

225. ***Mheshimwa Spika***, katika kipindi mwaka 2025/26, mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 1.15 ikijumuisha fedha za ndani shilingi milioni 705.4 na fedha za nje shilingi milioni 449.3. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imepokea kiasi cha shilingi milioni 119.6 ambapo fedha hizo zimetumika kuratibu Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto.

226. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Uhai na Maendeleo ya Mtoto (Child Survival and Development) ambapo Wizara imepokea fedha za nje kiasi cha **shilingi milioni 294.4** katika kuimarisha afua za kutoa elimu ya malezi chanya kwa watoto katika ngazi zote nchini. Aidha, Wizara imeratibu na kufanya Mkutano wa wadau wanaotekeleza afua za Vijana Balehe Nchini; kugharamia maandalizi ya mkutano wa Tano wa Nchi wanachama kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Afrika na Haki na Ustawi wa Mtoto; utekelezaji wa afua za Ulinzi na usalama wa mtoto Mtandaoni; kugharamia afua za MMMAM; na kuzuia aina zote za ukatili dhidi ya watoto ikiwemo ukeketaji na ukatili mitandaoni.

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI inatekeleza Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Advancing Gender Equality in Tanzania) unaojulikana kwa jina la "PAMOJA Project". Mradi huo unatakelezwa Tanzania Bara na Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano (5) na utagharimu Dola za Marekani milioni 100 kutoka Benki ya Dunia. Kati ya fedha hizo, Wizara imetengewa Dola za Marekani 38,000,000, OWM - TAMISEMI imetengewa Dola za Marekani 49,000,000 na Zanzibar imetengewa Dola za Marekani 13,000,000. Hata hivyo, Mradi huu ukitekelezwa ipasavyo, Serikali itapata ruzuku ya Dola za Marekani milioni nne.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wanawake waishio vijijini; kujenga vituo vya kulelea watoto wadogo mchana 200 (184 Tanzania Bara na 16 Zanzibar); kuwajengea wanaume uwezo na kuwa vinara wa kutokomeza ukatili wa kijinsia; ujenzi wa nyumba salama 10; na ujenzi na ukarabati wa Ofisi 40 za Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii.

229. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, mradi umetengewa Shilingi 6,576,717,000 ambapo hadi kufikia

Aprili 2026, jumla ya shilingi 5,836,716,758.67 zimetolewa. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya utambuzi wa maeneo ya ujenzi wa vituo vya kulelea Watoto wadogo mchana, nyumba salama na vikundi vitakavyonufaika na mikopo; kufanya utafiti wa msingi (baseline survey) ili kupata taarifa za awali kabla ya kuanza kutekeleza mradi; ununuzi wa magari sita (6); na kuandaa mifumo ya kuimarisha upatikanaji wa masoko kwa wajasiriamali na mifumo ya kidijitali ya kukusanya takwimu za mradi.

230. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii (Support to Social Welfare Services) ambapo katika kipindi cha mwaka 2025/26, kiasi cha **shilingi bilioni 3** kilitengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu ya vituo vya ustawi wa jamii. Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara, imepokea fedha kiasi cha **shilingi milioni 568.3** (Fedha za ndani shilingi milioni 500 na fedha za nje shilingi milioni 68.3) zilizotumika kuendeleza ujenzi wa Mahabusu ya Watoto Jijini Mwanza awamu ya pili; ukarabati wa miundombinu ya Mahabusu za Watoto Upanga, Mbeya, Mtwara na Kilimanjaro; ukarabati wa majengo na miundombinu ya umeme na mifumo ya vyoo katika makazi ya Wazee na Wasiojiweza Bukumbi,

Nyabange, Misufini, Kiilima, Magugu na Ipuli; na kufanya tathmini ya mifumo ya takwimu ya *Most Vulnerable Children Management Information Sytem (MVC – MIS)* na *Disctrict Case Management Information Sytem* (DCMIS).

## VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/27

### Mwelekeo wa Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii katika Mwaka 2026/2027

231. ***Mheshimiwa Spika,*** mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/27 umeandaliwa kwa kuzingatia misingi ifuatayo: -

i) DIRA 2050 inayosisitiza kuhusu Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii;

ii) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 inayoelekeza kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii;

iii) Mpango wa Taifa wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV), katika ya nguzo ya pili inayosisitiza kujenga uwezo wa watu na Maendeleo ya Kijamii;

iv) Mpango Mkakati wa Wizara na Mipango Mkakati ya Taasisi za Wizara kwa kipindi cha 2026/2027 – 2030/2031; na

v) Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27 pamoja na Sera, Sheria, Programu nyingine zinazotelezwa na Wizara.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itajikita katika maeneo machache yenye matokeo chanya kwa Taifa, uwezo wa kuleta mageuzi na mchango mkubwa katika kujenga Tanzania yenye jamii imara, jumuishi na yenye maendeleo endelevu. Hivyo, Wizara itatekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele saba (7) ambavyo ni:-

i) **Kujenga mtaji watu wa Taifa na kizazi cha Tanzania ya 2050**, kinachozingatia maadili, uzalendo, haki, usawa, ustawi na maendeleo jumuishi;

ii) **Kuimarisha huduma za ustawi, malezi na makuzi ya watoto, ulinzi wa kijamii na uthabiti wa Taifa** ili kuendeleza Taifa lenye mshikamano, ustahimilivu na utu wa kibinadamu kwa kuzingatia kuwa watu ndiyo mtaji mkuu wa Maendeleo ya Taifa;

iii) **Kuimarisha mifumo ya uwezeshaji wa wanawake, usawa wa kijinsia na kutokomeza ukatili wa kijinsia** ili kuhakikisha kuwa mwanamke anashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo;

iv) **Kufanya mageuzi ya uchumi wa makundi maalum na sekta isiyo rasmi kutoka uchumi wa kujikimu, kwenda uchumi rasmi wa kibiashara wenye tija, ushindani na wenye mchango katika pato la Taifa** kwa kuwa makundi hayo ni muhimu katika kujenga uchumi jumuishi;

v) **Kuimarisha matumizi ya kidijitali na takwimu katika huduma za kijamii ikihusisha uchambuzi wa takwimu** ili kurahisisha utendaji na kufanya maamuzi yenye ushahidi wa kitakwimu;

vi) **Kujenga jamii ya Kitanzania yenye amani, uwajibikaji na mshikamano** ili kuimarisha ushiriki wa wananchi katika maendeleo; na

vii) **Kuimarisha ushirikiano wa Kitaifa wa kimkakati kati ya Serikali, Asasi za Kiraia, Sekta binafsi, Taasisi za dini na wadau wa maendeleo** kwa kuwa maendeleo ya Taifa yanahitaji juhudi za pamoja.

233. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia vipaumbele hivyo, Serikali inalenga kujenga jamii imara na salama; wanawake wenye nguvu kiuchumi; watoto waliolelewa vyema; uchumi jumuishi na endelevu; jamii yenye maadili, mshikamano na amani ya kudumu; na Taifa lenye maendeleo yanayoongozwa na maarifa, teknolojia na ubunifu katika kufikia malengo ya DIRA 2050.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inapendekeza bajeti inayoweka vipaumbele katika ustawi na maendeleo ya jamii ikiwemo kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; huduma za watoto na wazee; ulinzi wa wanawake na wanaume; na makundi mengine maalumu kwa kuwa hizi si huduma za pembeni, bali ni **mfumo wa kulinda amani, usalama na uthabiti wa Taifa**. Hivyo, mafanikio ya bajeti hii hayatapimwa kwa kiasi cha fedha kilichotumika, bali kwa kiwango cha matokeo yaliyopatikana kwa familia, jamii/wananchi, Serikali na Taifa kwa ujumla.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii haulengi tu kutekeleza shughuli za Serikali, bali umeandaliwa mahsusi ili kuleta matokeo ya kimkakati yanayopimika yenye tija na mchango wa moja kwa moja wa kila mdau katika utekelezaji wa DIRA 2050. Lengo ni kuongeza ufanisi na uwajibikaji

katika utoaji huduma, kupunguza umaskini uliokithiri, kulinda makundi yaliyo hatarini, kujenga jamii salama, kuimarisha mshikamano wa Kitaifa na kujenga Taifa jumuishi.

236. ***Mheshimiwa Spika***, leo nasimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuzungumzia jambo moja kubwa sana ambalo linaamua mustakabali wa Taifa letu kuliko hata jambo jingine lolote. Na jambo lenyewe ni ***Malezi, Maadili, Makuzi na Ustawi wa Watoto wa Tanzania kwa Mwelekeo wa DIRA 2050.***

237. ***Mheshimiwa Spika,*** Tunaweza kujenga reli za kisasa, Tunaweza kujenga bandari kubwa, Tunaweza kujenga viwanja vya ndege, miji ya kisasa na uchumi mkubwa. Lakini tukishindwa kujenga mtoto wa Kitanzania mwenye maadili, nidhamu, uzalendo, utu na uwezo wa kuhimili ushindani wa dunia ya mwaka 2050 tutakuwa tumeshindwa kujenga Taifa imara.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sababu ukweli ni huu Taifa lolote hujengwa kwanza kwenye malezi kabla halijajengwa kwenye uchumi. Naomba Bunge hili Tukufu litambue kuwa mtoto wa leo ndiye Mtendaji wa Serikali wa kesho; Daktari wa kesho; Mwalimu wa kesho; Jaji wa kesho; Askari wa kesho; Mwekezaji wa Kesho na kiongozi wa Taifa wa

kesho. Kwa hiyo tukiharibu malezi ya mtoto leo, tutakuwa tumeharibu Tanzania ya mwaka 2050.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** leo Taifa letu linaanza kuona dalili ambazo hatupaswi kuzipuuza. Tunaona Kuporomoka kwa maadili katika jamii; Kuongezeka kwa ukatili dhidi ya watoto; Watoto kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya; Kuongezeka kwa mimba za utotoni; Athari kubwa za matumizi holela ya mitandao ya kijamii; Watoto kukosa malezi ya karibu; Kuongezeka kwa migogoro ya kifamilia; na kupungua kwa uwajibikaji wa pamoja katika malezi ya mtoto.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** jambo la kutisha zaidi siyo tu changamoto hizi kuwepo; jambo la kutisha zaidi ni pale jamii inaanza kuziona changamoto hizi kama ni mambo ya kawaida. Hapo ndipo Taifa huanza kupoteza mwelekeo wake wa maadili.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwelekeo wa DIRA 2050, Tanzania haiwezi kuwa Taifa lenye ushindani wa kimataifa kama Familia zitakuwa dhaifu; Malezi yatakuwa dhaifu; Watoto hawatakuwa salama na maadili yataendelea kuporomoka. DIRA 2050 inahitaji Taifa lenye watu wenye uwezo mkubwa wa kufikiri; Wenye nidhamu ya kazi; Wenye uzalendo; Wenye

maadili; Wenye afya ya akili na wenye uwezo wa kuishi katika ushindani wa dunia ya kisasa. Na msingi wa yote hayo unaanzia kwenye malezi ya mtoto.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** ni lazima sasa kama Taifa tufanye mabadiliko makubwa ya kimkakati katika eneo la malezi na ustawi wa watoto. Naomba nitoe maeneo sita (6) muhimu ambayo Taifa linapaswa kuyaangalia kwa uzito mkubwa:

243. ***Mheshimiwa Spika,*** moja, **Kurejesha Nguvu ya Familia**. Familia ndiyo taasisi ya kwanza ya Taifa. Mtoto wa Kitanzania hapaswi kulelewa na simu wala kulelewa na TikTok. Hapaswi kulelewa na mitandao ya kijamii bali Mtoto wa anahitaji Mzazi; Malezi; Muda; Maadili na uwepo wa familia. Ni lazima turejeshe mfumo wa wazazi kushiriki kikamilifu katika maisha ya watoto wao. Leo tuna Taifa ambalo linaanza kuwa na watoto wengi wenye mahitaji ya kiakili, kihisia na kimaadili kwa sababu ya kukosa malezi ya karibu.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** mbili, **Kujenga Mfumo wa Taifa wa Maadili**. Tukijenga uchumi bila maadili tutakuwa tumejenga hatari kubwa kwa Taifa. Tunapaswa kuwa na *National Moral Regeneration Programme;*

Mfumo wa Taifa wa Malezi; Kampeni ya Taifa ya Maadili na elimu ya maadili kuanzia ngazi za awali kabisa. Tunataka Watoto Wanaoheshimu Taifa lao; Wanaopenda kazi; Wenye utu; Wenye heshima na wanaolinda utamaduni wa Kitanzania.

245. ***Mheshimiwa Spika,*** tatu, **Kuimarisha Ulinzi wa Mtoto**. Mtoto anatakiwa kuwa salama Nyumbani; Shuleni; Kwenye mitandao; na katika jamii. Ni lazima tuimarishe madawati ya watoto; Mifumo ya kuripoti ukatili; Huduma za ushauri nasaha; Ulinzi wa mtoto mtandaoni na mifumo ya ufuatiliaji wa watoto waliyo kwenye mazingira hatarishi. Mtoto wa Tanzania hapaswi kuishi kwa hofu ndani ya Taifa lake mwenyewe.

246. ***Mheshimiwa Spika,*** nne, **Kuwekeza Kwenye Makuzi ya Awali ya Mtoto**. Tafiti zinasema ubongo wa mtoto unajengwa kwa asilimia 90 katika umri wa miaka 0 - 8. Tukiharibu hatua hiyo Taifa hupoteza ubunifu; Taifa hupoteza akili; Taifa hupoteza nguvu kazi; na Taifa hupoteza ushindani wa baadaye. Ni lazima tuwekeze zaidi katika Lishe ya mtoto; Afya ya mtoto; Elimu ya awali na mazingira bora ya ukuaji wa mtoto.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** tano, **Kulinda Afya ya Akili ya Watoto**. Dunia ya sasa imeleta changamoto mpya kwa watoto wetu. Watoto wengi wana msongo wa mawazo; Wanaishi kwenye upweke; Wanapitia ukatili wa kimtandao; na wengine wanakosa hata mtu wa kuwasikiliza. Tunapaswa kuanzisha mifumo imara ya mental wellness kwa watoto wetu.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** sita, **Kujenga Jamii Inayowajibika kwa Mtoto.** Malezi ya mtoto siyo jukumu la mzazi pekee. Ni jukumu la Serikali; Jamii; Viongozi wa dini; Walimu; Vyombo vya habari; na Taifa lote kwa ujumla. Tunapaswa kurejesha falsafa ya "Mtoto wa mmoja ni mtoto wa jamii."

249. ***Mheshimiwa Spika,*** Tukitaka kuondoa kero zilizopo leo kama vile Ukatili; Dawa za kulevya; Watoto wa mitaani; Mmomonyoko wa maadili; Uhalifu wa vijana; na changamoto za kijamii ni lazima tuanze na malezi. Kwa sababu matatizo mengi tunayoyaona leo yanaanzia kwenye kuporomoka kwa mfumo wa malezi.

250. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba niseme jambo moja kubwa mbele ya Bunge hili Tukufu "**Taifa lisipoamua kuwekeza kwa nguvu katika watoto wake leo, kesho litaingia gharama kubwa sana kurekebisha jamii**".

Tutatumia fedha nyingi Magerezani; katika vita dhidi ya dawa za kulevya; katika mapambano dhidi ya uhalifu; katika migogoro ya kijamii; na katika kurekebisha kizazi ambacho kingeweza kujengwa mapema. Ndiyo maana wahenga walisema "**Samaki mkunje angali mbichi**"

251. ***Mheshimiwa Spika,*** DIRA 2050 siyo tu kuhusu uchumi mkubwa. DIRA 2050 ni kuhusu kujenga Taifa lenye utu. Taifa lenye maadili; Taifa lenye watoto wenye ndoto; na Taifa lenye kizazi kinachojiamini. Na Taifa lenye watu wanaolitanguliza Taifa lao mbele ya maslahi binafsi. Naomba Bunge lako Tukufu, pamoja na Taifa letu, na kila mzazi wa Kitanzania tukubaliane jambo moja "**Hakuna uwekezaji mkubwa kwa Taifa kuliko uwekezaji kwa mtoto**." Na tukubaliane pia kuwa "**Malezi bora ya mtoto wa leo ndiyo usalama, maadili, amani, uchumi na mustakabali wa Tanzania ya mwaka 2050**."

252. ***Mheshimiwa Spika,*** kuna haja ya kukuza ujuzi wa wataalamu wa Ustawi na Maendeleo ya Jamii, hivyo, Wizara itajielekeza katika kuboresha dhana ya uanagenzi, ushirikishaji jamii na ubunifu kwa kutumia teknolojia rahisi ili kuleta ufumbuzi wa changamoto zilizopo kwenye jamii. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya Taasisi, vyuo na vituo vya kibunifu ili

kuwavutia vijana wengi kujiunga na masomo na kuongeza ushindani wa vyuo hivyo Kimataifa.

253. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuleta mageuzi yatakayochochea ukuaji wa uchumi jumuishi katika sekta isiyo rasmi, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta pamoja na wadau kufanya utambuzi, usajili na urasimishaji wa wafanyabiashara ndogondogo kijiditali. Lengo la hatua hii ni kupata takwimu sahihi za wafanyabiashara hao kupitia kanzidata iliyohuishwa na kuwaunganisha na fursa za kiuchumi.

254. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo. Aidha, Wizara itahamasisha uanzishwaji na uimarishwaji wa vikundi vya fedha ikiwemo SACCOS na VICOBA kwa lengo la kujenga utamaduni wa kuweka akiba na uwekezaji. Vilevile, Wizara itajielekeza katika kuwajengea uwezo wafanyabiashara ndogondogo kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali, elimu ya fedha, usimamizi wa biashara kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia za kidijitali.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara itahuisha na kuboresha Ajenda ya Taifa ya Kuwekeza katika Afya

na Maendeleo ya Vijana Balehe, sambamba na mwelekeo wa DIRA 2050 inayolenga kukuza ujuzi, ubunifu na matumizi ya teknolojia, hususan kwa vijana.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ongezeko la ukatili unaofanyika kupitia mitandao, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na wadau itaanzisha utaratibu maalum utakaowezesha kuchuja maudhui yasiyofaa kwa watoto. Sambamba na hilo, elimu kuhusu matumizi salama ya mitandao na uzuiaji wa ukatili itaendelea kutolewa kwa watoto, wazazi na walimu kupitia majukwaa mbalimbali, yakiwemo vyombo vya habari na taasisi za dini. Vilevile, mkakati wa usalama wa mtoto mtandaoni unaandaliwa ili kutoa mwongozo wa utekelezaji wa hatua hizi za kipaumbele, kwa lengo la kuhakikisha mazingira salama kwa watoto katika ulimwengu wa kidijitali na katika jamii kwa ujumla.

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma katika vituo vya Ustawi wa Jamii kwa makundi mbalimbali yenye uhitaji maalum wakiwemo wazee, watoto walio katika mazingira hatarishi, wananchi wasiojiweza, familia zenye migogoro, manusura wa ukatili wa kijinsia na watoto, pamoja na wananchi wenye changamoto za

afya ya akili na kisaikolojia. Huduma hizi zinalenga kuimarisha ustawi wa jamii, mshikamano wa kijamii na kuwawezesha wananchi kurejea katika maisha ya kawaida ili kushiriki shughuli za maendeleo.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la uwezeshaji wa wanawake kiuchumi halina maana kumkandamiza mwanaume bali ni kumtoa mwanamke kutoka nafasi ya mnufaika wa maendeleo, na kumpeleka kwenye nafasi ya mshiriki mkuu katika uzalishaji, uwekezaji, ubunifu, na uchumi wa Taifa. Katika kufanikisha hilo Wizara itajielekeza katika kuimarisha upatikanaji wa mikopo na teknolojia rahisi kwa wanawake ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma kupitia shughuli zao za ujasiriamali, sambamba na kuhamasisha matumizi ya biashara mtandao (e-commerce); na kujenga uwezo wa makundi maalum (wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu) kunufaika na fursa za uwezeshaji kiuchumi.

259. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na maamuzi, Wizara itaanzisha na kuendeleza programu atamizi za kuibua na kuendeleza viongozi wanawake na wasichana wanaochipukia ikiwa ni jitihada za kufikia malengo ya DIRA 2050 inayobainisha Tanzania kuwa kinara wa

usawa wa kijinsia barani Afrika na miongoni mwa nchi kumi duniani katika kupunguza pengo la kijinsia kwa asilimia 85.

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Washirika wa Maendeleo itaendelea kujenga uelewa wa ujumuishaji wa masuala ya kijinsia katika mchakato wa uandaaji wa mipango na bajeti za Wizara, Taasisi za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za mitaa (Gender Responsive Budgeting) kuhakikisha rasilimali za Taifa zinawanufaisha wanawake na wanaume kwa usawa.

261. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuweka mkazo katika kulinda haki na ustawi wa wajane kupitia Mwongozo wa Uratibu wa Huduma kwa Wajane (2025). Serikali itaimarisha mifumo ya uratibu wa huduma, ulinzi wa mirathi, pamoja na upatikanaji wa haki za msingi kwa kundi hili. Aidha, hatua mbalimbali zitachukuliwa kuhakikisha wajane wanapata huduma stahiki za kisheria, kijamii na kiuchumi, ili kuwawezesha kurejea katika maisha yenye tija na heshima.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaweka mkazo katika kuanzisha na kuimarisha vikundi vya wanaume vinavyolenga mabadiliko ya mitazamo na mila zinazokwamisha usawa wa kijinsia,

kuendesha kampeni za Kitaifa za uhamasishaji zinazowalenga wanaume na wavulana kuhusu wajibu wao katika kulinda haki za wanawake na kuzuia ukatili wa kijinsia, pamoja na kuwashirikisha kikamilifu katika programu za kiuchumi na kijamii ili kujenga mshikamano wa pamoja katika maendeleo.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi zinalenga kubadilisha dhana ya usawa wa kijinsia kutoka kuwa ajenda ya wanawake pekee na kuwa ajenda ya wote, ambapo wanaume wanakuwa washirika wa mabadiliko (change agent), hivyo kupunguza mitazamo hasi, kuimarisha ushirikiano ili kuwa na msingi imara wa jamii yenye usawa, amani na maendeleo endelevu.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** DIRA 2050 imeweka msisitizo mkubwa katika ushiriki thabiti wa wadau mbalimbali, zikiwemo Asasi za Kiraia na wananchi kwa ujumla, ambapo ushirikiano wa kimkakati baina ya wadau utaimarisha uratibu na kuhakikisha malengo ya kitaifa yanatimizwa kwa ufanisi. Aidha, DIRA 2050 imebainisha kuwa Asasi za Kiraia zina mchango muhimu katika kukuza demokrasia, kulinda haki za binadamu na kuchangia jitihada za kuboresha huduma za jamii.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia ubia na mahusiano kati ya Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 - 2026/27). Hatua hiyo inakwenda sambamba na mwelekeo wa DIRA 2050 inayohimiza upatikanaji wa rasilimali katika kutoa huduma jumuishi zikiwemo: hifadhi ya jamii, upatikanaji sawia wa maji safi, nishati na usafi wa mazingira, kuongezeka kwa ajira na kupunguza pengo la kijinsia, ambapo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni wadau muhimu na washirika katika kuchagiza utekelezaji wa afua hizo.

**Kazi Zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027**

266. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza vipaumbele, baadhi ya kazi zitakazotekelezwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (**Fungu 53**) katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni pamoja na:-

i) Kuboresha ustawi wa watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;

ii) Kutekeleza afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;

iii) Kufanya maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS) na Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabishara Ndogondogo (Wafanyabiashara Ndogondogo Management System - WBN – MIS);

iv) Kuendelea kuratibu utoaji wa mikopo kwa Wafanyabishara Ndogondogo, wanawake na makundi mengine nchini;

v) Kuandaa Kitabu cha Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2025;

vi) Kufanya tathmini na mapitio ya Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001) na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) na kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996);

vii) Kuanzisha mfuko wa pamoja wa ruzuku kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs Basket Fund);

viii) Kujenga Nyumba Salama 10 na vituo 184 vya kijamii vya kulelea watoto wadogo wa mchana wenye umri chini ya miaka 5;

ix) Kuimarisha majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi;

x) Kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati vya wanawake kila Mkoa;

xi) Kuhamasisha uanzishaji wa madawati ya ulinzi na usalama wa watoto katika shule za msingi na sekondari;

xii) Kuendeleza uanzishwaji wa madawati ya kuzuia ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi za Elimu ya juu na Kati; na Maeneo ya umma;

xiii) Kutoa elimu kuhusu wajibu wa msingi wa wazazi na walezi katika malezi chanya ya watoto;

xiv) Kuhamasisha matumizi salama ya mtandao kwa watoto kadi maalum za simu kwa watoto (Child SIM Card) zitakazosaidia kuchuja na kudhibiti maudhui yasiyofaa;

xv) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;

xvi) Kufanya Mapitio ya Mpango wa Kitaifa wa Uhamasishaji na Usimamizi wa Maendeleo Ngazi ya Msingi (*Bottom Up*);

xvii) Kuunganisha vyuo vinne (4) vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Jamii Ufundi kwenda Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru;

xviii) Kutoa huduma za msingi (chakula, mavazi, malazi na Matibabu) kwenye vituo 23 vya ustawi wa Jamii (Makazi ya Wazee 13, Mahabusu za watoto 7, Shule ya Maadilisho 1 na Makao ya Watoto 2);

xix) Kujenga Mfumo Jumuishi wa kidijitali wa Taarifa za Huduma za Ustawi wa Jamii (Comprehensive Social Welfare Information System); na Mfumo Jumuishi wa kidijitali wa Taarifa za Huduma za Maendeleo ya Jamii (Comprehensive Community Development Information System);

xx) Kuendelea na kampeni ya kuhamasisha ujenzi wa makazi bora ya gharama nafuu;

xxi) Kujenga makazi ya wazee ya kikanda katika Kanda ya Ziwa na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini;

xxii) Kuwajengea uwezo na kuwapatia vitendea kazi Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya msingi; na

xxiii) Kuhamasisha matumizi ya biashara mtandao kwa wanawake wajasiriamali ili kuongeza upatikanaji wa masoko.

267. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti hii ni mwelekeo wa kuwa na jamii imara, yenye kuthaminiana na inayojali utu kwa ustawi wa Taifa. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii unatarajiwa kuleta matokeo yafuatayo:

i) Kuongezeka kwa idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi;

ii) Kuongezeka kwa madawati na majukwaa ya kushughulikia matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto;

iii) Kuongezeka kwa idadi ya wanaume wanaoshiriki katika afua za kuzuia na kukabiliana na vitendo vya ukatili;

iv) Kuongezeka kwa fursa ya upatikanaji wa mikopo, mitaji na huduma za kifedha kupitia taasisi za fedha nchini;

v) Kuongezeka kwa idadi ya wanufaika wa mikopo yenye masharti nafuu kutoka Taasisi za fedha;

vi) Kuimarika kwa huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto, wazee na familia zenye dhiki;

vii) Kuongezeka kwa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa;

viii) Kuongezeka kwa idadi ya miradi inayotekelezwa kwa nguvu za wananchi;

ix) Uwepo wa Mifumo ya kidijitali ya kutoa huduma za Maendeleo na Ustawi wa jamii;

x) Uwepo wa Sera, mipango, sheria, miongozo iliyofanyiwa maboresho;

xi) Uwepo wa miundombinu iliyoboreshwa katika Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii;

xii) Kuongezeka kwa idadi ya vitendea kazi vya Maafisa Maendeleo ya jamii na Maafisa Ustawi wa jamii;

xiii) Ongezeko la vituo vya kijamii vya kulelea watoto wadogo mchana na uelewa wa

umuhimu wa huduma jumuishi za malezi kwa watoto Wadogo; na

xiv) Kuongezeka kwa idadi ya wazazi na walezi waliopata elimu kuhusu malezi chanya ya watoto katika zama za sasa.

268. ***Mheshimiwa Spika,*** DIRA 2050 haitajengwa kwa saruji na majengo pekee, bali itajengwa kwa watu wenye uwezo, jamii zenye mshikamano, wanawake wenye nguvu, watoto wenye maadili, uzalendo na wananchi wanaoshiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Na kwamba "Kupitia Wizara hii, Serikali inaendelea kujenga msingi wa Tanzania yenye ustawi, usalama wa kijamii, uchumi jumuishi na maendeleo endelevu kuelekea mwaka 2050."

## SHUKRANI

269. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta binafsi zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, Ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki kwa ushirikiano wanaotupatia ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

270. ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara ikiwa ni pamoja na: **Mashirika ya Kimataifa yakiwemo** UNICEF, UNFPA, UN-Women, WHO, UNDP, UNEP, IOM na UNESCO. Vilevile, ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Pia ninayashukuru **Mashirika ya Kimataifa** ambayo ni: - Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Enabel Foundation, Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation*. Aidha, ninazishukuru **Taasisi za Kifedha** za hapa nchini zinazoshirikiana na Wizara ambazo ni pamoja na Benki ya CRDB, Benki ya NBC, Benki ya NMB, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Benki ya Maendeleo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Benki ya Stanbic, Benki ya Azania, Benki ya Equity, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), *Akiba Commercial Bank* (ACB), Benki ya Biashara ya Dar es salaam (DCB) na Benki ya Mkombozi.

271. ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** na **Mashirika ya Dini** kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja

na; *Hope Four Young Girls Tanzania*, *World Vision, PACT Tanzania, HelpAge Tanzania, Compassion International*, *Responsible Organization Tanzania*, *Children in Crossfire*, *Railway Children Tanzania*, ICS, *SOS Children's Village Tanzania*, BRAC Maendeleo Tanzania, *Plan International - Tanzania*, Kivulini, C-SEMA; *Amani Girls*, Girls Effect na TECDEN, EGPAF.

272. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe pia shukrani zangu kwa Taasisi za Umma na sekta binafsi ikiwemo, TPA, PPRA, TPDC, WCF, UTT, TISEZA, Mgodi wa Geita (GGM), PMM Group, Bakhresa Group of Company, Total Energies, Asas Group of Company na Oryx Gas.

273. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nitoe shukrani zangu kwa **Jumuiya za makundi mbalimbali** ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Wizara. Jumuiya hizo ni pamoja na: - Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA), Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT), Jukwaa la ULINGO, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) na Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania (UMALITA).

274. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pongezi kwa mabinti zetu wa Timu ya mpira wa miguu ya wanawake chini ya miaka 20, (Tanzanite Queens), ambao wamefuzu na wataiwakilisha nchi katika mashindano ya kombe la Dunia yanayotarajia kufanyika kuanzia Septemba 5, 2026 nchini Poland. Tanzania ni moja kati ya nchi 4 za Afrika zitakazoshiriki mashindano hayo ya kuwania kombe la Dunia. ***Hakika Wanawake wameweza na hawajatuangusha***. Pia, navishukuru vikundi/kampeni za kijamii kama (Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), Lete Mabadiliko Chanya Ulipo (LeMaChu), Sauti ya Watoto Tanzania (SAWATA) pamoja na vyombo vyote vya habari.

275. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe shukrani zangu pia kwa viongozi na taasisi zetu za dini zikiwemo Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA).

276. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninaomba kuwashukuru Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO). Vilevile, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ninawashukuru sana Wakuu wa

Mikoa yote, Makatibu Tawala; Wakuu wa Wilaya; Wakurugenzi wa Halmashauri; na mitandao ya habari za kijamii ambao wamekuwa wakifuatilia na kutoa ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

277. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, hususan **Mume wangu mpendwa Wakili Msomi Methusela Gwajima** na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, ninawashukuru **wananchi wote wa Tanzania** kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa usawa wa jinsia huku wakitumia mawasiliano kupitia simu nilizozisema awali.

## MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2026/27

## MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2026/27

278. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara inatarajia kukusanya

maduhuli kiasi cha **shilingi bilioni saba, milioni arobaini, mia moja ishirini na tisa elfu** (shilingi 7,040,129,000) kutoka katika vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivyo ni pamoja na: Ada za wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Mitaala, Ada za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na Ada za mwaka za vituo vya kulelea watoto.

## MATUMIZI YA KAWAIDA

279. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2026/27, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **shilingi bilioni hamsini, mia moja thelathini na saba milioni, mia nane na moja elfu** (Shililngi 50,137,801,000) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni ishirini na tatu, milioni mia tatu kumi na tano, mia mbili na saba elfu** (shilingi 23,315,207,000) ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mia nane ishirini na mbili, mia tano tisini na nne elfu** (shilingi 26,822,594,000) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

## MIRADI YA MAENDELEO

280. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi bilioni hamsini na saba, milioni mia nane themanini na sita, mia nne**

**arobaini na mbili elfu** (shilingi 57,886,442,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni thelathini na sita, milioni mia tisa kumi na tano, mia nne na nne elfu** (Shilingi 36,915,404,000) ni Fedha za Ndani na **Shilingi bilioni ishirini, milioni mia tisa sabini na moja na thelathini na nane elfu** (shilingi 20,971,038,000) ni Fedha za Nje.

281. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** inaomba jumla ya **shilingi bilioni mia moja na nane, milioni ishirini na nne, mia mbili arobaini na tatu elfu** (shilingi 108,024,243,000) ili kutekeleza majukumu yake.

282. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum *www.jamii.go.tz.*

283. ***Mheshimiwa Spika,*** **Ninaomba Kutoa Hoja.**

**Kiambatisho Na.1***: Mchanganuo wa Mikopo ya Wafanyabiashara Ndogondogo kwa kila Mkoa kufikia Aprili, 2026.*

| Na | Mkoa | Wanufaika kwa Jinsi | | | Kiasi cha Mkopo kwa Kila Jinsi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ke | Me | Jumla | Ke | Me | Jumla |
| 1. | Dar es Salaam | 312 | 458 | 770 | 824,500,000 | 1,215,800,000 | 2,040,300,000 |
| 2. | Arusha | 401 | 205 | 606 | 964,000,000 | 475,500,000 | 1,439,500,000 |
| 3. | Kilimanjaro | 336 | 204 | 540 | 807,450,000 | 483,300,000 | 1,290,750,000 |
| 4. | Morogoro | 285 | 313 | 598 | 523,653,022 | 588,920,000 | 1,112,573,022 |
| 5. | Ruvuma | 205 | 158 | 363 | 462,800,000 | 383,000,000 | 845,800,000 |
| 6. | Mwanza | 193 | 164 | 357 | 457,300,000 | 385,400,000 | 842,700,000 |
| 7. | Mbeya | 242 | 172 | 414 | 475,700,000 | 359,800,000 | 835,500,000 |
| 8. | Mara | 260 | 148 | 408 | 492,550,000 | 304,600,000 | 797,150,000 |
| 9. | Mtwara | 168 | 215 | 383 | 346,900,000 | 445,000,000 | 791,900,000 |
| 10. | Tanga | 187 | 186 | 373 | 353,650,000 | 376,600,000 | 730,250,000 |
| 11. | Lindi | 224 | 217 | 441 | 340,170,000 | 380,950,000 | 721,120,000 |
| 12. | Pwani | 169 | 135 | 304 | 357,600,000 | 311,500,000 | 669,100,000 |
| 13. | Dodoma | 187 | 134 | 321 | 354,700,000 | 283,800,000 | 638,500,000 |
| 14. | Shinyanga | 171 | 117 | 288 | 347,950,000 | 288,100,000 | 636,050,000 |
| 15. | Iringa | 141 | 125 | 266 | 255,200,000 | 288,700,000 | 543,900,000 |
| 16. | Manyara | 133 | 82 | 215 | 296,900,000 | 195,550,000 | 492,450,000 |
| 17. | Songwe | 113 | 89 | 202 | 277,200,000 | 194,400,000 | 471,600,000 |
| 18. | Tabora | 126 | 134 | 260 | 214,980,000 | 242,950,000 | 457,930,000 |
| 19. | Njombe | 120 | 62 | 182 | 261,800,000 | 144,100,000 | 405,900,000 |
| 20. | Singida | 123 | 114 | 237 | 190,750,000 | 202,500,000 | 393,250,000 |
| 21. | Kagera | 93 | 95 | 188 | 180,700,000 | 204,600,000 | 385,300,000 |
| 22. | Geita | 69 | 84 | 153 | 171,700,000 | 198,500,000 | 370,200,000 |
| 23. | Simiyu | 87 | 74 | 161 | 165,900,000 | 145,250,000 | 311,150,000 |
| 24. | Kigoma | 97 | 73 | 170 | 157,400,000 | 150,700,000 | 308,100,000 |
| 25. | Rukwa | 41 | 65 | 106 | 86,300,000 | 158,160,000 | 244,460,000 |
| 26. | Katavi | 37 | 83 | 120 | 46,200,000 | 133,800,000 | 180,000,000 |
| | **Jumla** | **4,520** | **3,906** | **8,426** | **9,413,953,022** | **8,541,480,000** | **17,955,433,022** |

***Chanzo; NMB Bank Aprili, 2026***

***KIAMBATISHO NA. 2:* IDADI YA WATOTO WALIOFANYIWA UKATILI WA KIJINSIA (KINGONO) NA AINA ZINGINE ZA UKATILI KWA AINA YA KOSA JANUARI – DESEMBA, 2024 NA 2025.**

***A. Idadi ya watoto waliofanyiwa ukatili wa kijinsia (kingono)***

| Na. | SHTAKA | 2024 | | | 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wavulana | Wasichana | JUMLA | Wavulana | Wasichana | JUMLA |
| 1. | Kubaka | - | 6,888 | 6,888 | - | 6,500 | 6,500 |
| 2. | Kulawiti | 1,586 | 142 | 1,728 | 1,327 | 222 | 1,549 |
| 3. | Shambulio la aibu | 76 | 582 | 658 | 83 | 629 | 712 |
| 4. | Kuzini na maharimu | 5 | 34 | 39 | 3 | 33 | 36 |
| 5. | Kumpa mwanafunzi mimba | - | 1,624 | 1,624 | - | 1,105 | 1,105 |
| **JUMLA** | | **1,667** | **9,270** | **10,937** | **1,413** | **8,489** | **9,902** |
| **B.** | **Aina zingine za ukatili kwa aina ya kosa** | | | | | | |
| 1. | Kutupa watoto | 99 | 72 | 171 | 93 | 72 | 165 |
| 2. | Wizi wa watoto | 42 | 35 | 77 | 56 | 30 | 86 |
| 3. | Kutelekeza mtoto | 21 | 61 | 82 | 49 | 88 | 137 |
| | **JUMLA** | **162** | **168** | **330** | **198** | **190** | **388** |

**Chanzo**; *Jeshi la Polisi: Takwimu za hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani Januari - Desemba 2024 na 2025.*

**Kiambatisho Na.3:** Namba za simu za Mawasiliano na Maafisa Ustawi katika Kila Mkoa




NAMBA ZA SIMU ZA MAAFISA USTAWI WA JAMII WA MIKOA YOTE 26 NCHINI

0677200372 – Arusha
0677200373 – Dar es Salaam
0677200374 – Dodoma
0677200375 – Geita
0677200376 – Iringa
0677200377 – Kagera
0677200378 – Katavi
0677200379 – Kigoma
0677200381 – Kilimanjaro
0677200382 – Lindi
0677200383 – Manyara
0677200384 – Mara
0677200385 – Mbeya
0677200386 – Morogoro
0677200387 – Mtwara
0677200388 – Mwanza
0677200389 – Njombe
0677200391 – Pwani
0677200392 – Rukwa
0677200393 – Ruvuma
0677200394 – Singida
0677200395 – Simiyu
0677200396 – Songwe
0677200397 – Shinyanga
0677200398 – Tabora
0677200399 – Tanga

Maendeleo ya Jamii Jamii Yetu Tanzania // www.jamii.go.tz

***KIAMBATISHO NA.4:* IDADI YA WATU WAZIMA WALIOFANYIWA UKATILI WA KIJINSIA (KINGONO) KWA AINA YA KOSA JANUARI – DESEMBA, 2024 NA 2025**

| Na. | SHITAKA | 2024 | | | 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Wanaume** | **Wanawake** | **JUMLA** | **Wanaume** | **Wanawake** | **JUMLA** |
| 1. | Kubaka | - | 7,712 | 7,712 | - | 7,219 | 7,219 |
| 2. | Kulawiti | 1,573 | 161 | 1,734 | 1,398 | 252 | 1,650 |
| 3. | Shambulio la aibu | 200 | 1,313 | 1,513 | 170 | 1,420 | 1,590 |
| 4. | Kumpa mwanafunzi mimba | - | 1,790 | 1,790 | - | 1,166 | 1,166 |
| | **JUMLA** | **1,773** | **10,976** | **12,749** | **1,568** | **10,057** | **11,625** |

**Chanzo**; *Jeshi la Polisi: Takwimu za hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani Januari- Desemba 2024 na 2025.*




***Jengo la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum lililopo Mji wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma.***